NOVEMBA 17, 2026

/islamicftz

VISION 2050

IMAAN

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

ISSN 5618 - NO. 611

Mwinyi aeleza fursa mpya za ushirikiano na Oman



Vipaumbele vitano kukuza uwekezaji halali nchini

Cifca, Shirkah waomba sheria ya fedha za Kiislamu, Sukuk ya Serikali



Mafuriko yaongeza mateso Gaza, familia 46,000 zaathirika

Da'awah ya Sheikh Twaha kuimarisha Imani, Amani na Maadili Jijini Arusha



Matarajio makubwa kwa Kadhi Mkuu mpya Kenya



Mwanzo mpya wa maridhiano ya kitaifa



Rais Samia apendekeza kuanzishwa tume maalumu kuratibu maridhiano ya kujenga umoja wa kitaifa na maandalizi ya mageuzi ya Katiba.

Uchumi wa Halal si mpango wa kueneza dini

Ni fursa ya biashara inayozingatia ubora, usafi, uadilifu na uzalishaji wenye maadili, kwa kuzingatia misingi inayozingatia Sharia

Samia aanzisha safari ya maridhiano ya kitaifa

Rais Samia akutana na viongozi wa vyama vya siasa na kuwaambia ni wakati wa kuunda Tume ya Maridhiano na Upatanishi ikiwa ni mwanzo wa safari ya Katiba mpya.

Rais Samia Suluhu Hassan amependekeza kuanzishwa kwa Tume ya Maridhiano na Usuluhishi itakayoratibu maandalizi ya mchakato wa marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akisisitiza umuhimu wa mazungumzo jumuishi katika kujenga umoja wa kitaifa.

Rais Samia alitoa pendekezo hilo alipokutana na wajumbe wa Baraza la Vyama vya Siasa katika Ikulu ya Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuendeleza mashauriano na wadau mbalimbali kuhusu mustakabali wa nchi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ikulu, Rais alisema ni wakati wa kuendeleza mazungumzo na wadau wa kisiasa, mashirika ya kiraia pamoja na sekta binafsi kwa lengo la kuimarisha misingi ya taifa.

Alisema kuanzishwa kwa tume hiyo kutasaidia kuratibu maandalizi ya mchakato wa kupitia Katiba na kuweka mazingira bora ya kufanikisha maridhiano miongoni mwa Watanzania.

Pendekezo hilo linakuja baada ya kuongezeka kwa wito wa maridhiano kufuatia maandamano ya Oktoba 29, 2025, yaliyogeuka kuwa vurugu na kusababisha vifo vya watu wasiopungua 518 pamoja na uharibifu wa mali za umma na binafsi.

Baada ya matukio hayo, Rais Samia aliunda Tume ya Uchunguzi kuchunguza kilichotokea. Miongoni mwa mapendekezo ya tume hiyo ilikuwa kuanzishwa kwa Tume ya Maridhiano kwa ajili ya kuimarisha mshikamano wa kitaifa, sambamba na Tume ya Uchunguzi wa Jinai.

Julai mwaka huu, Rais aliteua Tume ya Uchunguzi wa Jinai na kueleza dhamira yake ya kuanzisha pia Tume ya Maridhiano ili kuharakisha mchakato wa marekebisho ya Katiba.

Akizungumza na viongozi wa vyama vya siasa Julai 30, 2026, alisema serikali haitasubiri kukamilika kwa uchunguzi wote kabla ya kuanza hatua za maridhiano.

Akizungumzia mkutano wa jana, Katibu Mkuu wa AAFP, Rashid Rai, alisema Rais aliwajulisha viongozi wa vyama kuwa tume hiyo itaundwa na inatarajiwa kutangazwa hivi karibuni.

Alisema vyama vya siasa vitakuwa na wawakilishi saba, watano kutoka vyama vya CCM, Chadema, ACT-Wazalendo, CUF na Chaumma, kila kimoja kikiwasilisha mwakilishi mmoja.

Wawakilishi wawili waliobaki watatoka katika vyama vingine 14, ikiwemo AAFP.

Rai alisema Rais amesisitiza kuwa Chadema haiwezi kuachwa nje ya mchakato huo licha ya kutohudhuria mkutano huo, kutokana na ukubwa wake na mchango wake katika siasa za nchi.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa DP, Abdul Mluya, alisema Rais amewaahidi kuwa tume hiyo itatangazwa hivi karibuni na kuhakikisha makundi yote yanawakilishwa kwa haki.

Alisema Rais pia atakutana na makundi mengine ili kupata maoni yatakayosaidia kuunda chombo jumuishi.

Naye Katibu Mkuu wa NRA, Almas Kisabya, alisema marekebisho ya Katiba hayawezi kufanyika bila mazungumzo, akieleza kuwa hatua zinazochukuliwa na Rais zinaonesha dhamira ya kujenga taifa lenye umoja.



JINSI PENDEKEZO LA MARIDHIANO LILIVYOKUWA NA KUENDELEZWA

Oktoba 29, 2025
Maandamano yaliyohusishwa na Uchaguzi Mkuu yageuka kuwa vurugu, yakiongeza wito wa maridhiano ya kitaifa.

Agosti 7, 2026
Rais Samia aunda Tume ya Uchunguzi kuhusu matukio ya Oktoba 2025.

Julai 30, 2026
Rais Samia akutana na viongozi wa vyama vya siasa Ikulu na kusema maandalizi ya maridhiano hayapaswi kusubiri kukamilika kwa kazi ya Tume ya Uchunguzi wa Jinai.

Novemba 15, 2026
Samia apendekeza kuundwa kwa Tume ya Maridhiano na Usuluhishi kuratibu maandalizi ya marekebisho ya Katiba.

Da’awah ya Sheikh Twaha kuimarisha Imani, Amani na Maadili Jijini Arusha

Katika kuhuisha imani, kuimarisha maadili na kuhamasisha jamii kushikamana na Qur’an na Sunnah, Sheikh Ibrahim Twaha anatarajia kuongoza ziara maalumu ya kida’wah jijini Arusha.

Katika kuendeleza juhudi adhimu za kuenenda kwenye misingi ya Qur’an na Sunnah, na kuimarisha ng uzo za udugu wa Kiislamu, Mkurugenzi wa Taasisi tukufu ya The Islamic Foundation ya Morogoro, Sheikh Ibrahim Twaha, anatarajia kuongoza ziara maalum ya kida’wah jijini Arusha. Ziara hii inalenga kuleta mwamko wa kiroho, kutoa mwongozo sahihi wa kimaadili kwa jamii, na kujibu changamoto za kiakili na kifikra zinazowakabili vijana na jamii kwa ujumla.

Ratiba ya ziara hiyo iliyosheheni mafunzo ya kina itaanza Alhamisi, tarehe 19/11, ambapo Sheikh Ibrahim Twaha atatoa muhadhara mkubwa katika Msikiti wa Kaloleni. Muhadhara huu unatazamiwa kuwakutanisha Waislamu kutoka pembe mbalimbali za jiji hilo ili kujifunza kuhusu misingi imara ya kushikamana na uongofu wa Mtume Muhammad (S.A.W) katika zama hizi za changamoto.

Siku ya Ijumaa, tarehe 20/11, shughuli za kida’wah zitashika kasi pale Sheikh atakapotoa Khutba ya Ijumaa katika Msikiti wa Qiblatein. Hii ni fursa adhimu kwa waumini kupata nasaha zenye kugusa mioyo na kuelekeza jamii katika utendaji wa mema na ukataji wa maovu. Baada ya Swala ya Magharibi siku hiyo hiyo, muhadhara mwingine mzito utatolewa katika Msikiti wa Mtendeni, ukiwaalika vijana na wazee kusikiliza mawaidha yatakayojenga fikra sahihi za Kiislamu.

Kilele cha hamasa ya kielimu kitafikiwa Jumamosi, tarehe 21/11, kupitia semina maalum ya vijana wa vyuo vikuu itakayofanyika katika Chuo cha Ufundi Arusha (ATC). Semina hii ni ngao muhimu kwa kizazi kipya cha wasomi, ikilenga kuwapa miongozo ya kukabili changamoto za kimaadili, misimamo ya kiimani, na kujenga mustakabali unaoendana na maadili ya Kiislamu huku wakisaka elimu ya dunia.

Hatimaye, Jumapili, tarehe 22/11, ziara hiyo itafungwa kwa mtindo wa kipekee kupitia muhadhara wa kinamama utakaofanyika katika Ukumbi wa Arusha Mall. Wanawake wa Kiislamu, wakiwa kama nguzo kuu ya malezi na utunzaji wa misingi ya familia, watapata fursa ya kunufaika na nasaha zitakazoelekeza nafasi yao tukufu katika jamii kwa mujibu wa Shariah.

Kwa ujumla, shughuli hizo zinalenga kuendeleza juhudi za kuifikisha elimu ya Kiislamu kwa makundi mbalimbali ya jamii, kwa kuzingatia kuwa Da’awah ni jukumu la kuelimisha, kukumbusha na kuelekeza watu katika kheri kwa hekima na nasaha njema.





Rais Mwinyi aishukuru Zayed, UAE kwa kuimarisha elimu Zanzibar

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, ametoa shukrani kwa Taasisi ya Zayed na Ubalozi wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) nchini Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Zanzibar katika kuimarisha sekta ya elimu, akisema ushirikiano huo una mchango mkubwa katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kuongeza fursa za vijana kupata ujuzi wa kitaalamu.

Dkt. Mwinyi amesema Serikali ya Awamu ya Nane itaendelea kuwekeza katika ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya skuli, sambamba na kuimarisha elimu ya ufundi na mafunzo ya amali ili kuhakikisha wananchi wanapata elimu bora na vijana wanakuwa na ujuzi unaokidhi mahitaji ya soko la ajira na uchumi wa kisasa.

Alitoa kauli hiy, wakati akiweka mawe ya msingi ya ujenzi wa Skuli ya Msingi Mtopepo na karakana nne za kisasa za uhandisi katika Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (KIST), Mkoa wa Mjini Magharibi.

Amesema Serikali imejipanga kuendelea kujenga skuli za kisasa zenye miundombinu inayowezesha utoaji wa elimu yenye ubora, ikiwemo uwepo wa maabara na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), ili kuwaandaa wanafunzi kukabiliana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Alieleza kuwa Skuli ya Msingi Mtopepo itakayojengwa kwa ghorofa nne, ikiwa na jumla ya madarasa 50 na lifti, ni sehemu ya juhudi za Serikali kuhakikisha wanafunzi wanapata mazingira bora, salama na rafiki ya kujifunzia.

Alisema uwekezaji katika miundombinu ya elimu ni hatua muhimu katika kujenga msingi imara wa maendeleo ya Zanzibar, kwani unasaidia kuongeza fursa za kupata elimu na kuinua ubora wa rasilimali watu.

Katika hatua nyingine, Dkt. Mwinyi alisema ujenzi wa karakana nne za kisasa katika KIST utasaidia kuimarisha elimu ya ufundi kwa kuwapa wanafunzi nafasi ya kupata mafunzo ya vitendo yanayowaandaa kukabiliana na changamoto halisi za maeneo yao ya kazi.

Alizitaja fani zitakazohusishwa na karakana hizo kuwa ni Uhandisi wa Ujenzi, Uhandisi wa Mitambo, Useremala na Ufundi wa Magari, ambazo zina nafasi muhimu katika kukuza uzalishaji, ujasiriamali na maendeleo ya sekta mbalimbali za uchumi.

Alisisitiza kuwa elimu ya ufundi na mafunzo ya amali ni nyenzo muhimu katika kupunguza changamoto ya ajira kwa vijana, kwa kuwajengea uwezo wa kujiajiri au kuajiriwa kulingana na mahitaji ya soko.

Aidha, aliwataka wakandarasi wanaosimamia miradi hiyo kuhakikisha wanatekeleza kazi kwa kuzingatia mikataba, viwango vya ubora na muda uliopangwa, akisisitiza kuwa Serikali inatarajia kuona miradi hiyo inakamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma zilizokusudiwa.

Alisema uwekezaji huo unaakisi dhamira ya Serikali ya kuimarisha sekta ya elimu kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na ya baadaye, huku akibainisha kuwa ushirikiano na wadau wa maendeleo ni muhimu katika kufanikisha azma hiyo.

Dkt. Mwinyi amesisitiza kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi katika kuimarisha huduma za kijamii, hususan elimu, ili kujenga jamii yenye maarifa, ujuzi na uwezo wa kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Zanzibar.

TANZANIA HALA INVESTMENT SUMMIT

CIFCA
مركز مراقبة المعاملات المالية الإسلامية والإستشارات
Centre for Islamic Finance Compliance and Advice

Shirkah

NA
Yusufu Amini
0787 503 085

Vipaumbele vitano kukuza uwekezaji halali nchini



Naibu Waziri wa Fedha, Mhandisi Mshamu Ally Munde (katikati) Mwenyekiti wa CIFCA, Aref Nahdi (kushoto), na Salum Awadh wa Shirkah katika Kongamano la Kwanza la Uwekezaji Halali Tanzania, lililofanyika Novemba 12, 2026, katika Hoteli ya Hyatt Regency, Dar es Salaam.

- Wadau wahimiza sheria ya fedha za Kiislamu, Sukuk ya Serikali
- PBZ Ikhlas yaeleza mchango wake kukuza uwekezaji halali nchini
- Cifca, Shirkah waomba sheria ya fedha za Kiislamu, Sukuk ya Serikali
- CMSA: Hakikini leseni za washauri wa uwekezaji kuepuka matapeli
- Mtambalike alia na mtazamo potofu sekta fedha za Kiislamu, elimu isambazwe

TANZANIA HALA INVESTMENT SUMMIT

CIFCA Centre for Islamic Finance Compliance and Advice

Shirkah

NA
Ukhti Fatima SS
0789 201 383



Vipaumbele vitano kukuza uwekezaji halali nchini

Serikali imezitaka taasisi za fedha za Kiislamu kuweka mkazo katika vipaumbele vitano vya kimkakati, ikiwemo kuvutia mitaji kutoka ndani na nje ya nchi, kubuni bidhaa mpya za uwekezaji na kuelekeza fedha katika sekta za uzalishaji ili kuongeza mchango wa uwekezaji halali katika uchumi.

Vipaumbele hivyo vilitajwa na Naibu Waziri wa Fedha, Mhandisi Mshamu Ally Munde, wakati akifungua Kongamano la Kwanza la Uwekezaji Halali Tanzania, lililofanyika Novemba 12, 2026, katika Hoteli ya Hyatt Regency, Dar es Salaam.

Munde, aliyemwakilisha Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar, alisema Serikali inatarajia Shirkah Asset Management na Kituo cha Ushauri na Uzingatiaji wa Fedha za Kiislamu (CIFCA), kwa kushirikiana na wadau wengine, kutekeleza vipaumbele hivyo.

Kipaumbele cha kwanza, alitaja, ni kuvutia mitaji kutoka ndani na nje ya nchi kwa kujenga ushirikiano wa kimkakati na mitandao ya wawekezaji, hususan katika masoko ya kimataifa ya fedha za Kiislamu, ili kugharamia shughuli za kiuchumi.

Vilevile, alitaka kuongezwe bidhaa za uwekezaji zinazozingatia Shariah ili kukidhi mahitaji ya watu binafsi, wafanyabiashara na wawekezaji wa kitaasisi, pamoja na kuwavutia wanaoepuka baadhi ya huduma za kifedha kutokana na imani zao.

Katika kipaumbele cha tatu, alitaka mitaji ielekezwe katika sekta za uzalishaji, hususan miundombinu, kilimo, viwanda, nishati na utalii, ili kufadhili miradi yenye tija na kuchangia malengo ya maendeleo.

Kadhalika, alisisitiza elimu ya fedha kwa wananchi kuhusu uwekezaji halali na fursa zake huku kipaumbele cha tano akitaja kuwa ni kuimarisha utawala bora na uzingatiaji wa Shariah kwa kuhakikisha uwazi, uwajibikaji na usimamizi madhubuti ili kuongeza ushindani na imani ya wawekezaji.

Serikali yaahidi kuboresha mazingira

Munde alisema Serikali itaendelea kuboresha sera, sheria, kanuni na usimamizi ili kuchochea uwekezaji na kulinda masilahi ya wawekezaji huku pia akitambua nafasi ya uwekezaji halali katika kuwanufaisha watu wote bila kujali dini zao, mradi uzingatie sheria na Shariah.

Kwa mujibu wa takwimu alizowasilisha, mwaka 2025 benki za Kiislamu zilichangia asilimia 3 ya amana na asilimia 2.6 ya mikopo katika sekta ya benki, huku Sukuk zikivutia maombi ya uwekezaji ya Sh bilioni 601.3.

Alihimiza vyuo kuimarisha mafunzo ya fedha za Kiislamu ili kuongeza wataalamu wazawa, huku akielezea matumaini yake kuwa Tanzania inaweza kuwa kitovu cha uwekezaji unaozingatia Shariah Afrika Mashariki kwa kuimarisha sera na taasisi.

Kongamano hilo liliandaliwa na Shirkah Asset Management, CIFCA na Taqseem Academy kujadili fursa za uwekezaji halali katika kufanikisha Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

TANZANIA HALA INVESTMENT SUMMIT

CIFCA Centre for Islamic Finance Compliance and Advice

Shirkah

NA
Yusufu Amini
0787 503 085

Wadau wahimiza sheria ya fedha za Kiislamu, Sukuk ya Serikali

Wakizungumza, Mwenyekiti wa Kituo cha Ushauri na Uzingatiaji wa Fedha za Kiislamu (CIFCA), Sheikh Aref Nahdi, na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirkah Asset Management, Salum Awadh, wakati wa Kongamano la Uwekezaji Halali Tanzania (Tanzania Halal Investment Summit 2026)





Serikali imeombwa kuharakisha kupitishwa kwa sheria ya fedha za Kiislamu na kutoa Sukuk ya Serikali Tanzania Bara ili kupanua fursa za uwekezaji, kukusanya mitaji na kuongeza mchango wa sekta hiyo katika maendeleo ya uchumi wa taifa.

Wito huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Kituo cha Ushauri na Uzingatiaji wa Fedha za Kiislamu (CIFCA), Sheikh Aref Nahdi, na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirkah Asset Management, Salum Awadh, wakati wa Kongamano la Uwekezaji Halali Tanzania (Tanzania Halal Investment Summit 2026), lililofanyika Novemba 12, katika Hoteli ya Hyatt Regency, Dar es Salaam.

Akizungumza kabla ya kumkaribisha mgeni rasmi, Naibu Waziri wa Fedha, Mhandisi Mshamu Ally Munde, Sheikh Nahdi aliiomba Serikali kuharakisha mchakato wa kupitisha sheria hiyo, akisema suala hilo limekuwa likisubiriwa kwa muda mrefu.

"Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi sitaki kuchosha zaidi, lakini tunaomba tu kwamba utakapotoka hapa pia utusaidie kuisukuma sheria ya fedha za Kiislamu Tanzania ili iweze kupita bungeni. Hili ni la muda mrefu sana," alisema.

Kwa upande wake, Awadh, akiwasilisha mada kuhusu hali ya fedha za Kiislamu Afrika Mashariki, alipendekeza Serikali kutoa Sukuk Tanzania Bara na kuweka mazingira ya kodi yenye usawa kati ya bidhaa za fedha za Kiislamu na zile za kawaida.

Alisema hatua hizo zinapaswa kwenda sambamba na kuimarisha mazingira ya kisheria na ushirikiano baina ya Serikali, mamlaka za udhibiti, taasisi za fedha na wawekezaji.

Fursa kubwa ya kiuchumi

Katika wasilisho lake, Awadh alionyesha kuwa Tanzania imepiga hatua katika kuendeleza huduma za fedha za Kiislamu kupitia benki, masoko ya mitaji na kuimarishwa kwa mfumo wa udhibiti.

Alisema Sukuk zilivutia maombi ya uwekezaji ya zaidi ya Sh bilioni 600 nchini mwaka 2025, jambo linaloonyesha uwezo wa mfumo huo kukusanya mitaji.

Kwa upande wa Afrika Mashariki, alitaja Kenya kuwa na benki tatu kamili za Kiislamu, huku Uganda ikianza kujenga sekta hiyo baada ya Salaam Bank kuanza kutoa huduma mwaka 2024. Awadh alisema Tanzania ina nafasi ya kutumia fedha za Kiislamu kuchangia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, inayolenga kujenga uchumi wenye thamani ya dola trilioni moja.

Alieleza kuwa Sukuk zinaweza kutumika kugharamia miradi mikubwa ya miundombinu, ikiwemo barabara, bandari, umeme na maji, wakati mifumo mingine ya fedha za Kiislamu inaweza kusaidia uwekezaji katika kilimo, makazi na biashara ndogo na za kati.

Alisisitiza kuwa fedha za Kiislamu hazipaswi kutazamwa kama huduma za benki pekee, bali kama mfumo mpana wa uwekezaji unaoweza kutumiwa na watu wote, bila kujali dini zao.

Changamoto

Awadh alisema licha ya maendeleo yaliyopatikana sekta ya fedha za Kiislamu bado inakabiliwa na changamoto zinazohitaji juhudi za pamoja ili kuzitatua ikiwemo uhaba wa Sukuk zinazotolewa na Serikali na kampuni binafsi, udogo wa soko la upili la Sukuk na ukosefu wa nyenzo za kusimamia ukwasi wa benki zinazozingatia Shariah.

Alisema changamoto nyingine ni uelewa mdogo wa wananchi kuhusu huduma za fedha za Kiislamu na pia upungufu wa wanazuoni wenye utaalamu wa Shariah katika masuala ya fedha, wabunifu wa bidhaa na wataalamu wenye mafunzo ya viwango vya kimataifa.

Akizungumzia hatua zinazohitajika kutoka sekta binafsi, Awadh alisema taasisi za fedha na wawekezaji zinapaswa kuanzisha mifuko zaidi ya uwekezaji halali na kutumia teknolojia kurahisisha wananchi kupata huduma hizo.

TANZANIA HALA INVESTMENT SUMMIT

CIFCA Centre for Islamic Finance Compliance and Advice

Shirkah

NA
Ukhti Fatima SS
0789 201 383

Mtambalike alia na mtazamo potofu sekta fedha za Kiislamu, elimu isambazwe

DAR ES SALAAM. Mwekezaji na mfanyabiashara, Jumanne Rajab Mtambalike, amesema mtazamo potofu wa jamii kuhusu fedha za Kiislamu ni miongoni mwa vikwazo vinavyokwamisha matumizi ya huduma hizo nchini, akitaka elimu kuhusu mfumo huo isambazwe zaidi.

Alisema baadhi ya wananchi wanadhani huduma hizo ni kwa ajili ya Waislamu pekee au zinahusu benki tu, hivyo kushindwa kutambua fursa zake katika biashara na uwekezaji.

Akichangia mjadala kuhusu mitaji kwa biashara ndogo na za kati katika Kongamano la Uwekezaji Halali Tanzania, Mtambalike alisema jamii inapaswa kuelewa kuwa huduma hizo zinaweza kutumiwa na watu wote, bila kujali dini zao.

Alisema bidhaa za fedha za Kiislamu zinapaswa kutambulishwa kwa kuonyesha manufaa yake, ikiwemo masharti rafiki, gharama zinazovutia na ulinzi wa masilahi ya wahusika, badala ya kusisitiza utambulisho wa kidini.

Mtambalike alisema elimu ya fedha za Kiislamu haipaswi kuishia benki na taasisi rasmi za fedha, kwa kuwa shughuli nyingi za biashara na uwekezaji hufanyika nje ya taasisi hizo.

Katika maelezo yake, Mtambalike pia alisema bidhaa za fedha za Kiislamu lazima ziwe na gharama zinazoweza kushindana sokoni, akieleza kuwa mfanyabiashara anaweza kushindwa kuchagua mtaji unaozingatia Shariah ikiwa gharama yake ni kubwa. Alisisitiza kuwa biashara inayotafuta uwekezaji lazima iwe na mfumo imara, mpango unaotekelezeka na uwezo wa kuzalisha faida, kwani wawekezaji huzingatia pia hatari na tija, si Shariah pekee.

Sukuk fursa ya kuvutia mitaji kutoka nje – Rashid H. Rashid

DAR ES SALAAM. Tanzania imeshauriwa kutumia Sukuk na bidhaa nyingine za fedha za Kiislamu kuvutia mitaji kutoka nje ya nchi, hususan mataifa ya Ghuba, ili kuongeza fedha za kugharamia miradi ya maendeleo.

Ushauri huo ulitolewa na Mkuu wa Kitengo cha Benki ya Kiislamu cha CRDB, Rashid H.H. Rashid, wakati wa Kongamano la Uwekezaji Halali Tanzania, lililofanyika Novemba 12, 2026, jijini Dar es Salaam. Rashid alisema nchi za Ghuba zina mitaji mikubwa inayotafuta fursa za uwekezaji, hivyo Tanzania inaweza kutumia Sukuk, hati za uwekezaji zinazozingatia Shariah, kuvutia sehemu ya fedha hizo.

"Lazima tuweke mkazo katika kuvutia mitaji kutoka nchi za nje. Kupitia Sukuk na bidhaa nyingine zinazozingatia Shariah, tuna nafasi nzuri ya kupata mitaji kutoka masoko ya kimataifa, hususan nchi za Mashariki ya Kati," alisema.

Alisisitiza umuhimu wa kuimarisha mazingira ya kisheria na udhibiti, pamoja na kuhakikisha utulivu na kanuni zinazotabirika ili kujenga imani ya wawekezaji wa kimataifa.

Akizungumzia ujumuishaji wa kifedha, Rashid alisema Sukuk zinaweza kuwavutia wawekezaji wanaoepuka hati fungani za kawaida kutokana na kutokidhi matakwa ya Shariah, hivyo kupanua wigo wa wawekezaji na uwezo wa kukusanya mitaji.

Akitoa mfano, alisema Sukuk ya CRDB Al Barakah ya mwaka 2025 ilivutia maombi ya uwekezaji ya zaidi ya Sh bilioni 210, dhidi ya lengo la awali la takribani Sh bilioni 45 hadi 50.

Rashid pia aliishauri Serikali kutoa Sukuk Tanzania Bara kwa ajili ya kugharamia miradi mikubwa ya miundombinu, akisema hatua hiyo inaweza kuchangia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Kamugisha, mfano hai uwekezaji halali hauna mipaka ya dini

DAR ES SALAAM. Mkurugenzi wa Alpha Capital, Gervase Kamugisha, amesema uwekezaji unaozingatia Shariah hauwahusu Waislamu pekee, akitumia uzoefu wake wa kuanzisha Alpha Halal Fund kuonyesha kuwa mfumo huo unaweza kuendeshwa na watu wa dini tofauti.

Akizungumza katika Kongamano la Uwekezaji Halali Tanzania, lililofanyika Novemba 12, 2026, Dar es Salaam, Kamugisha alisema kampuni yake ilianzisha mfuko huo kwa kuvutiwa na misingi ya maadili na uwajibikaji, si msukumo wa imani ya kidini.

Alisema uamuzi huo uliibua maswali kutoka kwa Waislamu na wasiokuwa Waislamu.

"Nikizungumza nina Alpha Halal Fund nikienda kanisani kwangu, watu wanasema, 'Hii si ya Waislamu hiyo?' Lakini pia kwa upande wa pili, 'Tangu lini askofu akasimamia mfuko wa uwekezaji?'" alisema. Kamugisha alieleza kuwa uzingatiaji wa Shariah unategemea mifumo madhubuti ya usimamizi, ukaguzi na utekelezaji wa masharti, si dini ya wanaoendesha kampuni.

Makamu Mwenyekiti wa CIFCA, Mohammed Hafidh, alimpongeza Kamugisha kwa hatua hiyo, akisema: "Bila ya kujali imani ya mtu, ametuonyesha kwamba kizuri kinajiuza na kimemvutia."

Katika mchango wake, Kamugisha alisema mifuko ya uwekezaji wa pamoja inayozingatia Shariah inawawezesha wananchi wenye mitaji midogo, hata ya Sh 200,000 au Sh 300,000, kuunganisha fedha zao na kushiriki katika miradi mikubwa ambayo wasingeweza kuigharamia mmoja mmoja.

Dkt. Huda aeleza faida za uwekezaji katika uchumi halisi

DAR ES SALAAM. Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Dkt. Huda Ahmed Yussuf, amesema uwekezaji katika sekta halisi za uchumi una manufaa mapana kwa jamii, ikiwemo kuongeza uzalishaji, ajira na upatikanaji wa bidhaa na huduma.

Akizungumza katika Kongamano la Uwekezaji Halali Tanzania, lililofanyika Novemba 12, 2026, Dar es Salaam, Dkt. Huda alisema moja ya sifa muhimu za fedha za Kiislamu ni kuunganisha shughuli za kifedha na uzalishaji halisi.

Alieleza kuwa uwekezaji katika kilimo, viwanda na miundombinu unaweza kuchochea shughuli nyingine za kiuchumi, tofauti na uwekezaji unaolenga zaidi mabadiliko ya bei za mali za kifedha.

"Unapowekeza moja kwa moja kwenye uchumi halisi, unazalisha ajira, lakini pia uzalishaji wa bidhaa na huduma unaongezeka," alisema. Dkt. Huda alizitaka taasisi kubwa za uwekezaji, ikiwemo mifuko ya hifadhi ya jamii, kuzingatia faida za kifedha na manufaa ya kijamii.

TANZANIA HALA INVESTMENT SUMMIT

CIFCA Centre for Islamic Finance Compliance and Advice

Shirkah

NA
Yusufu Amini
0787 503 085

Sheikh Issa: Maeneo 4 yanayokosekana sekta ya fedha za Kiislamu nchini

Tanzania imetajwa kuwa na mapungufu katika maeneo manne muhimu ya fedha za Kiislamu, hali inayopunguza fursa za uwekezaji, upatikanaji wa mitaji na ufanisi wa huduma za kifedha.

Maeneo hayo ni mifuko ya uwekezaji katika majengo, soko la fedha za muda mfupi, soko la bidhaa na teknolojia za fedha za Kiislamu.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti Mtendaji wa Yusra Sukuk, Sheikh Mohammed Hemed Issa, katika Kongamano la Uwekezaji Halali Tanzania, lililofanyika Novemba 12, 2026, Dar es Salaam.



Alisema licha ya Tanzania kupiga hatua katika benki za Kiislamu, Takaful, Sukuk na mifuko ya uwekezaji halali, bado haijajenga mfumo kamili wa kuendeleza sekta hiyo.

Eneo la kwanza ni mifuko ya uwekezaji katika majengo (Islamic REITs), inayowawezesha watu kuunganisha mitaji na kuwekeza katika majengo yanayozalisha mapato, kama nyumba za kupangisha, maghala na hospitali, bila kila mmoja kununua jengo lake.

Sheikh Issa aliitaka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kuweka mazingira ya kuanzisha mifuko hiyo.

Eneo la pili ni soko la fedha za muda mfupi linalowezesha benki za Kiislamu kupata au kuwekeza fedha kwa mikataba inayozingatia Shariah. Alisema mfumo huo ungesaidia benki kusimamia ukwasi na kupata fedha zinapokabiliwa na upungufu wa muda mfupi, akitaka Benki Kuu kushughulikia suala hilo.

Eneo la tatu ni soko la bidhaa, hususan mazao ya kilimo, linaloweza kuwawezesha wakulima kupata mitaji kabla ya mavuno kupitia mikataba halali ya mauzo, huku likirahisisha biashara inayozingatia Shariah.

Eneo la nne ni teknolojia za fedha za Kiislamu (Islamic fintech), zinazorahisisha uwekezaji, bima ya Takaful na miamala ya kidijitali. Alisema licha ya juhudi za kampuni kama Shirkah, huduma hizo zinahitaji kupanuliwa.

Akitoa mifano ya kimataifa, Sheikh Issa aliitaja Malaysia, yenye mifuko ya uwekezaji katika majengo tangu 2006, soko la fedha za Kiislamu la muda mfupi tangu 1994 na mfumo wa biashara ya bidhaa unaozingatia Shariah.

Katika changamoto nyingine, Sheikh Issa alitaja tofauti za tafsiri za Shariah kuwa changamoto inayowachanganya wateja, akisema wakati mwingine bidhaa iliyothibitishwa kuwa halali na wataalamu fulani hupingwa na wengine.



NA
Ukhti Fatima SS
0789 201 383

Muro ataja njia za SMEs kupata mitaji halali

DAR ES SALAAM. Wafanyabiashara wadogo na wa kati (SMEs), hususan wanawake, wameshauriwa kutumia akaunti za benki na mifumo ya kidijitali kurekodi miamala yao ili kuongeza nafasi ya kupata mitaji inayozingatia Shariah, huku mifumo ya ubia ikitajwa kuwa fursa nyingine ya kupata fedha.

Ushauri huo ulitolewa na Mkuu wa Kitengo cha Sahl Banking katika KCB Bank Tanzania, Amour Muro, na Sheikh Khalfan Abdallah, wakati wa Kongamano la Uwekezaji Halali Tanzania, lililofanyika Novemba 12, 2026, Dar es Salaam.

Akijibu swali la mwanzilishi wa Zari's Taste, Zainab Shomari, kuhusu namna mwanamke anayehitaji Sh 150,000 kwa biashara ya maandazi anavyoweza kupata mtaji bila riba, Muro alisema changamoto kubwa ni ukosefu wa dhamana, historia ya biashara na taarifa zinazothibitisha mapato.

Alisema mfanyabiashara wa maandazi au vitumbua anaweza kufungua akaunti ya benki kidijitali na kupitisha mapato yake humo ili kujenga historia ya miamala inayoweza kusaidia benki kutathmini uwezo wake wa kupata ufadhili.

Muro alisema benki zina bidhaa zinazozingatia Shariah, zikiwemo Murabahah, ambapo benki hununua bidhaa na kumuuzia mteja kwa faida iliyokubaliwa, na Ijarah, inayohusu ukodishaji wa mali.

CMSA: Hakikini leseni za washauri wa uwekezaji kuepuka matapeli

DAR ES SALAAM. Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) imewataka wananchi kuhakiki leseni za washauri na taasisi za uwekezaji kabla ya kutumia huduma zao ili kujiepusha na watoa huduma wasioidhinishwa.

Wito huo ulitolewa na mwakilishi wa CMSA, Aisha, wakati wa Kongamano la Uwekezaji Halali Tanzania, lililofanyika Novemba 12, 2026, Dar es Salaam.

Akijibu swali kuhusu upatikanaji wa washauri wa kitaalamu, Aisha alisema CMSA ina rejista ya watoa huduma wenye leseni katika tovuti yake, inayowawezesha wananchi kuthibitisha uhalali wao.

"Unaweza kuingia kwenye tovuti ya CMSA, kuna rejista ya wenye leseni wote," alisema.

Alieleza kuwa rejista hiyo inajumuisha washauri wa uwekezaji, madalali na majukwaa ya kuchangisha mitaji yaliyoidhinishwa, huku wananchi wakiweza pia kuwasiliana na CMSA kwa ufafanuzi.

Kuhusu gharama, alisema ada za washauri hutegemea makubaliano na wateja, kulingana na aina na ukubwa wa huduma.

PBZ Ikhlas yaeleza mchango wake kukuza uwekezaji halali nchini

DAR ES SALAAM. Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), kupitia PBZ Ikhlas, imesisitiza dhamira yake ya kukuza uwekezaji halali kwa kufadhili biashara, miundombinu na kupanua huduma za fedha zinazozingatia Shariah.

Akizungumza katika Kongamano la Uwekezaji Halali Tanzania, Novemba 12, 2026, mwakilishi wa PBZ, Rajab Mohammed Ramia, alisema benki hiyo inatoa huduma za akaunti za akiba na hundi, ufadhili wa nyumba, viwanja na biashara ndogo na za kati kupitia mikataba inayozingatia Shariah, ikiwemo Tawarruq na Commodity Murabaha.

PBZ Ikhlas ilikuwa mdhamini mkuu wa kongamano hilo.

Rajab alisema PBZ inaendeleza Wakfu wa Fedha (Cash Waqf), ikiwemo ushirikiano na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), uliotangazwa Aprili 2026.

Alitaja Zanzibar Treasury Sukuk 1 ya mwaka 2025 kuwa mfano wa uwekezaji halali, huku akieleza kuwa majadiliano kuhusu miamala ya kimataifa ya Sukuk yanaendelea.

Alisema PBZ inashirikiana na Serikali za Muungano na Zanzibar kufadhili miradi ya barabara, shule na majengo ya biashara.

Aliwakaribisha wananchi kutumia huduma za benki hiyo Tanzania Bara na Zanzibar.

Uaminifu watajwa kuwa nguzo muhimu ya uwekezaji halali

DAR ES SALAAM. **Wataalamu wa fedha za Kiislamu wamewataka wawekezaji na wasimamizi wa mitaji kuzingatia uaminifu, uwazi na kuheshimu mikataba, wakisema misingi hiyo ni nguzo muhimu katika kukuza uwekezaji halali, kulinda mali na kujenga imani kati ya washirika wa kibiashara.**

Wakizungumza katika Kongamano la Uwekezaji Halali Tanzania lililofanyika Novemba 12, 2026, jijini Dar es Salaam, wataalamu hao walisema kuwa upatikanaji wa mitaji pekee hauwezi kuhakikisha mafanikio ya uwekezaji ikiwa hautaambatana na uadilifu, uwajibikaji na usimamizi unaozingatia maadili.

Walisema kuwa katika mfumo wa uchumi wa Kiislamu, uaminifu si suala la kimaadili pekee, bali ni wajibu unaopaswa kuzingatiwa katika kila hatua ya biashara, kuanzia makubaliano ya awali, matumizi ya fedha hadi ugawaji wa faida na hasara.

Sheikh Khalfan Abdallah alisema uaminifu ni msingi wa mikataba ya ubia, hususan Mudarabah, inayowaunganisha wenye mitaji na wafanyabiashara kwa lengo la kuendesha shughuli za kiuchumi kwa makubaliano maalumu.

Alisema katika mfumo huo, mwenye mtaji hukabidhi fedha kwa mjasiriamali au mfanyabiashara mwenye ujuzi wa kuendesha biashara, huku pande hizo zikikubaliana namna ya kugawana faida itakayopatikana.

Alisisitiza kuwa ni muhimu kila upande kutekeleza wajibu wake kwa uaminifu na kuheshimu masharti yaliyokubaliwa, akieleza kuwa kuvunja makubaliano au kutumia vibaya fedha za uwekezaji kunaweza kuharibu mahusiano ya kibiashara na kupunguza imani ya wawekezaji.

Kwa upande wake, Sheikh Yassir Masoud alisema biashara halali inapaswa kujengwa katika misingi ya ukweli na uwazi, akieleza kuwa mtu anayekabidhiwa kusimamia mtaji wa mwingine ana wajibu wa kutoa taarifa sahihi kuhusu matumizi ya fedha na matokeo ya uwekezaji.

Akirejea hadithi ya Swahaba Urwah al-Bariqi, alieleza umuhimu wa uaminifu katika shughuli za biashara na wajibu wa kutenda haki katika kusimamia mali za watu wengine.

Alisema ukosefu wa uwazi katika taarifa za kifedha unaweza kusababisha migogoro kati ya wawekezaji na wasimamizi wa mitaji, hivyo ni muhimu kuwepo kwa mawasiliano ya wazi na taarifa zinazoweza kuthibitishwa.

TANZANIA HALA INVESTMENT SUMMIT

CIFCA Centre for Islamic Finance Compliance and Advice

Shirkah



MATUKIO
KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar
0655 763 580

Kongamano la Kwanza la Uwekezaji Halali Tanzani











Kongole, matarajio makubwa kwa Kadhi Mkuu mpya Kenya

Pongezi zimeendelea kutolewa kwa Kadhi Mkuu mpya wa Kenya, Sheikh Hassan Omar Daffa, huku matarajio makubwa yakielekezwa kwake katika kuimarisha utoaji haki, uadilifu na umoja wa jamii ya Kiislamu nchini humo.

Miongoni mwa waliompongeza ni Jaji Mkuu wa Kenya, Martha Koome, na Waziri wa Madini na Uchumi wa Bahari, Hassan Joho, ambao wamesisitiza umuhimu wa hekima, uadilifu na uwajibikaji katika kutekeleza majukumu yake mapya.

Koome amesema Daffa ana uzoefu mkubwa wa kimahakama, elimu ya sheria na maarifa ya kina ya sheria za Kiislamu, mambo anayotarajia yatamsaidia kuongoza Mahakama za Kadhi kwa hekima na uadilifu.

Katika ujumbe wake wa pongezi, Koome amesisitiza kuwa Ofisi ya Kadhi Mkuu ina nafasi ya kipekee katika mfumo wa Katiba na utoaji haki nchini Kenya.

Amesema uongozi wa ofisi hiyo unahitaji si maarifa ya sheria pekee, bali pia unyenyekevu, huruma na uelewa wa kina wa mahitaji ya jamii inayohudumiwa.

Kwa upande wake, Joho amemuombea Daffa hekima, subira na nguvu za kutekeleza majukumu yake kwa haki, huku akieleza matumaini kwamba uongozi wake utaimarisha umoja wa Waislamu.

Daffa, aliyeteuliwa Ijumaa, Novemba 13, na Tume ya Huduma za Mahakama (JSC), anarithi nafasi iliyoachwa wazi baada ya kifo cha Kadhi Mkuu wa zamani, Sheikh Abdul-Halim Hussein, Julai 2025.

Tangu Agosti mwaka jana, Sheikh Sukyan Hassan Omar alikuwa akikaimu nafasi hiyo, hivyo uteuzi wa Daffa unamaliza kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja bila Kadhi Mkuu wa kudumu.

Kadhi Mkuu mpya anakabiliwa na jukumu la kusimamia Mahakama za Kadhi zinazoshughulikia mashauri ya ndoa, talaka, mirathi na hadhi binafsi kwa mujibu wa sheria za Kiislamu.

Kwa mujibu wa Ibara ya 170 ya Katiba ya Kenya ya mwaka 2010, mamlaka ya mahakama hizo yanahusu mashauri ambayo pande zote ni Waislamu na zimekubali kuwasilisha mgogoro wao katika Mahakama za Kadhi.

Hivyo, miongoni mwa matarajio yanayomkabili Daffa ni kuhakikisha huduma hizo zinatolewa kwa haki, bila upendeleo, huku akijenga imani ya wananchi katika mfumo wa mahakama.

"Daffa ambaye kabla ya uteuzi huo alikuwa Kadhi Mwandamizi (Principal Kadhi), ana shahada ya uzamili katika misingi ya sheria za Kiislamu na shahada ya kwanza ya Sharia na Masomo ya Kiislamu kutoka Chuo Kikuu cha Umm Al-Qura, Saudi Arabia.

Pia ana shahada ya sheria kutoka Chuo Kikuu cha Mount Kenya na ni wakili wa Mahakama Kuu ya Kenya.

Uteuzi wake ulifuatia mchakato wa ushindani uliohusisha waombaji 14, ambapo tisa walichaguliwa kwa usaili uliofanyika Novemba 2 na 3.

Kwa Tanzania, uteuzi huo unaibua mjadala mpana kuhusu nafasi ya Mahakama za Kadhi katika utoaji haki kwa Waislamu Afrika Mashariki.

Wakati Kenya inazitambua Mahakama za Kadhi kupitia Katiba yake, Zanzibar ina mfumo rasmi wa mahakama hizo, huku Tanzania Bara ikiwa haina mfumo wa aina hiyo licha ya Waislamu kuidai kwa muda mrefu.

Kwa Daffa, changamoto kubwa sasa si kupata wadhifa, bali kuonyesha kupitia utendaji wake kwamba Mahakama za Kadhi zinaweza kuendelea kuwa sehemu muhimu ya utoaji haki unaoaminika na jamii.



خطبة الجمعة

MIMBARI ZETU

IMEANDALIWA
Na Barnabas Mkwayu
0766 364 354



Sheikh Zuberi: Misikiti ni nyumba za Allah, vituo vya malezi na amani, tuitunze

Sheikh Zuberi: Misikiti ni nyumba za Allah, vituo vya malezi na amani, tuitunze

Amiri wa Baraza la Sunni Tanzania (Basuta), Sheikh Ali Zuberi, amewataka Waislamu kuthamini na kuitunza misikiti kwa kuhakikisha inatimiza dhima yake ya kumuabudu Allah (Subhanahu Wa Ta'ala), kulea nafsi na kujenga jamii yenye maadili mema.

Akizungumza katika hotuba ya Swala ya Ijumaa iliyoswaliwa katika Msikiti wa Al-Ghaith, unaomilikiwa na Taasisi ya The Islamic Foundation, Sheikh Zuberi amesema msikiti una nafasi kubwa katika maisha ya Muislamu, hivyo haupaswi kutazamwa kama jengo la kutekeleza ibada ya Swala pekee.

Amesema misikiti ni vituo muhimu vya malezi ya kiroho, kuimarisha undugu, mshikamano na kuwaongoza waumini katika maisha yanayozingatia mafundisho ya Qur'ani Tukufu na Sunna za Mtume Muhammad (Rehema na amani zimshukie).

Ameeleza kuwa Allah (Subhanahu Wa Ta'ala) anapenda misikiti, akisisitiza kuwa hadhi ya nyumba hizo inaonekana pia katika historia ya Uislamu, ikiwamo Kaaba iliyoko Makka, ambayo ndiyo nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya watu kumuabudu Allah.


"Msikiti ni sehemu ambayo Allah Subhanahu Wa Ta'ala anaipenda sana. Ni nyumba ya Allah, lakini pia ina malengo ya kuwalea Waislamu kiroho. Mtu anayeingia ndani ya msikiti anapaswa kupata amani," amesema.

Ameongeza kuwa msikiti una jukumu la kumjenga Muislamu kuwa mtu mwema, mwenye utulivu na anayezingatia amani katika maisha yake na jamii inayomzunguka.

Kwa mujibu wa Sheikh Zuberi, msikiti unapaswa kuwa mahali pa kuwalea watu katika misingi ya amani ya Allah, kuanzia katika nafsi zao hadi katika makazi na mahusiano yao na wengine.

Amesisitiza kuwa hata mtu aliyekuwa akijihusisha na makosa anapoingia msikitini, anapaswa kupata fursa ya kujifunza, kujirekebisha na kurejea katika njia iliyonyooka.

Amesema dhima hiyo inaonyesha kuwa misikiti ina nafasi pana katika kujenga jamii bora, kwa kuwa malezi yanayotolewa ndani yake yanapaswa kuzaa waumini wenye kumcha Allah, kuheshimu haki za wengine na kuishi kwa amani. Aidha, amewahimiza Waislamu kushiriki katika kuitunza misikiti, kuheshimu utukufu wake na kuhakikisha inakuwa mazingira salama ya ibada, elimu na malezi kwa vizazi vya sasa na vijavyo.



MIMBARI ZETU

خطبة الجمعة

MSIKITI MTAKATIFU, MAKKA

IMAMU NA KHATIBU SHEIKH DKT. BANDAR BIN ABDULAZIZ BALILA



Khatibu wa Makka: Tawhid si ibada pekee, ni mfumo mzima wa maisha

MAKKA, Saudi Arabia. Imamu na Khatibu wa Msikiti Mtukufu wa Makka, Sheikh Dkt. Bandar bin Abdulaziz Balila, amewataka Waislamu kuilinda na kuimarisha imani ya Tawhid, akisisitiza kuwa kumpwekesha Allah (Subhanahu Wa Ta'ala) si suala la ibada pekee, bali ni msingi unaopaswa kuongoza kauli, itikadi, matendo na miamala ya kila siku.

Akitoa khutba ya Swala ya Ijumaa, Novemba 13, 2026, Sheikh Balila alisema neema ya Uislamu na imani ya Tawhid ni miongoni mwa neema kubwa zaidi alizowajalia Allah wanadamu, hivyo kila Muislamu ana wajibu wa kuzilinda na kuzithamini.

Alieleza kuwa Tawhid ndiyo haki ya Allah kwa waja Wake na msingi mkuu wa maisha ya mwanadamu, akibainisha kuwa ndiyo sababu ya kuumbwa kwa viumbe, kuteremshwa kwa vitabu vya mbinguni na kutumwa kwa Mitume ili kuwaongoza watu katika njia iliyonyooka.

Alisisitiza kuwa kumpwekesha Allah hakupaswi kuishia katika kutekeleza ibada kama Swala, bali kunapaswa kuonekana katika mwenendo mzima wa Muislamu, ikiwamo namna anavyozungumza, anavyoamini, anavyotenda na kushughulika na watu wengine.

Katika hatua nyingine, Sheikh Balila alionya dhidi ya kumshirikisha Allah na viumbe Wake, akieleza kuwa kufanya hivyo ni dhambi kubwa inayopingana moja kwa moja na msingi wa Tawhid.

Alikumbusha kuwa hakuna kiumbe anayeweza kuleta manufaa au madhara kwa mwingine bila idhini ya Mwenyezi Mungu, bila kujali cheo, uwezo au hadhi aliyonayo katika jamii.

Kutokana na umuhimu huo, aliwataka Waislamu kujilinda wenyewe na familia zao dhidi ya itikadi, kauli na matendo yanayoweza kuathiri usahihi wa imani yao, huku wakihakikisha wanamtegemea Allah katika mambo yote ya maisha. Aidha, aliwahimiza waumini kuwafikishia wasiokuwa Waislamu ujumbe wa Tawhid kwa hekima, upole na mawaidha mazuri, wakieleza uzuri wa Uislamu na manufaa ya kumpwekesha Allah katika maisha ya duniani na Akhera.

Katika kuhitimisha mawaidha yake, Sheikh Balila aliwasisitiza Waislamu kumcha Allah, kuongeza toba, kuwa na ikhlasi katika ibada na kuimarisha uhusiano wao na Muumba wao.

MSIKITI WA MTUME, MADINA

IMAM NA KHATIBU SHEIKH DKT. ABDULMUHSIN BIN AL-QASIM



Khatibu wa Madina akumbusha hesabu ya Kiyama, haki za wengine

MADINA, Saudi Arabia. Imamu na Khatibu wa Msikiti wa Mtume (Rehema na amani zimshukie), Sheikh Dkt. Abdulmuhsin bin Muhammad Al-Qasim, amewakumbusha Waislamu kuwa kila mwanadamu atasimama mbele ya Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama kujibu kuhusu imani yake, matendo na neema alizojaliwa katika maisha ya duniani.

Akitoa khutba ya Swala ya Ijumaa, Novemba 13, 2026, Sheikh Al-Qasim alisema maandalizi ya siku hiyo yanahitaji kila Muislamu kuimarisha imani, kutenda mema na kumcha Allah (Subhanahu Wa Ta'ala) katika hali zote, awe faraghani au mbele ya watu.

Alieleza kuwa kuamini Siku ya Mwisho ni miongoni mwa misingi mikuu ya imani ya Kiislamu, akibainisha kuwa kifo si mwisho wa maisha ya mwanadamu, bali ni mwanzo wa safari ya kuelekea maisha ya Akhera.

Alisisitiza kuwa kaburi ni hatua ya kwanza katika safari hiyo, ambapo mwanadamu atakutana na maswali kuhusu Mola wake, dini yake na Mtume wake, kabla ya kusimama mbele ya Allah kwa ajili ya kuhesabiwa matendo yake.

Sheikh Al-Qasim alisema hesabu ya Siku ya Kiyama haitahusu ibada na matendo binafsi pekee, bali itajumuisha pia utekelezaji wa ahadi, mikataba, haki za watu wengine na majukumu ambayo mwanadamu alikabidhiwa katika maisha yake.

Akizungumzia hali ya mwanadamu anapokaribia kufa, alieleza tofauti kati ya roho ya muumini na ya mtu asiyeamini, akisisitiza kuwa imani na mwenendo wa mwanadamu vina nafasi muhimu katika kuamua hatima yake ya maisha ya Akhera. Aidha, alizungumzia neema kubwa ambazo Allah amewaandalia watu wa Peponi, akitaja kupata radhi za Mwenyezi Mungu na neema ya kumuona Allah kuwa miongoni mwa malipo makubwa zaidi kwa waumini.

Katika kuhitimisha khutba yake, Sheikh Al-Qasim aliwahimiza Waislamu kujihesabu kabla hawajahesabiwa, kushikamana na mafundisho ya Qur'an Tukufu na Sunnah za Mtume Muhammad (Rehema na amani zimshukie), kutekeleza haki za wengine na kuepuka dhuluma.

Aref Nahdi: Tumieni vyombo vya habari vya Imaan kuelimisha umma



Mwenyekiti wa Taasisi ya The Islamic Foundation, Aref Nahdi, amelitaka Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuimarisha ushirikiano na vyombo vya habari vya Imaan katika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu shughuli, huduma na usalama wa reli nchini.

Nahdi alitoa wito huo alipokutana na kufanya mazungumzo na baadhi ya watendaji wa TRC katika makao makuu ya taasisi hiyo mjini Morogoro.

Katika mazungumzo hayo, aliipongeza TRC kwa juhudi zake za kuboresha huduma za usafiri wa reli, akisema miradi na maboresho yanayoendelea yana mchango mkubwa katika kurahisisha usafiri, kukuza shughuli za kiuchumi na kuchochea maendeleo ya wananchi.

Aidha, aliilitaka shirika hilo kutumia vyombo vya habari vya Imaan, vinavyomilikiwa na The Islamic Foundation, kutoa elimu kuhusu masuala mbalimbali ya reli, ikiwemo umuhimu wa kulinda miundombinu ya reli ya kisasa (SGR) na reli ya kawaida (MGR) dhidi ya vitendo vinavyoweza kuhatarisha usalama na uendelevu wa huduma.

Alisisitiza kuwa ushirikiano kati ya TRC na vyombo vya habari ni muhimu katika kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu wajibu wao wa kulinda miundombinu ya umma na kutambua mchango wa sekta ya reli katika maendeleo ya taifa.

Kabla ya mazungumzo hayo, watendaji wa TRC walishiriki katika kipindi maalumu cha Ghuba ya Imaan kupitia Radio Imaan FM, ambapo walitoa elimu kuhusu Kampeni ya Usalama wa Treni, majukumu na huduma za shirika hilo, pamoja na mipango na maboresho yanayoendelea katika sekta ya reli nchini.

Kwa upande wao, watendaji wa TRC wameeleza kufurahishwa na mapokezi waliyoyapata na fursa ya kutumia vyombo vya habari vya Imaan kuwafikia wananchi.

Walisema ushirikiano huo utasaidia kusambaza taarifa sahihi na kuongeza uelewa wa jamii kuhusu usalama wa reli na huduma zinazotolewa na shirika hilo.

WHO yaitaja Tanzania miongoni mwa vinara wa tiba za dharura

Shirika la Afya Duniani (WHO) limeichagua Tanzania kushiriki mpango wa kuimarisha huduma za tiba ya dharura na kupanua upatikanaji wake, hasa maeneo ya pembezoni, ili kuokoa maisha. Nchi nyingine zilizochaguliwa ni Ethiopia, Rwanda na Uganda.

Akizungumza Arusha katika Mkutano wa Nane wa Afrika wa Tiba ya Dharura (AfCEM), Kiongozi wa Mpango wa ACTxBEC kutoka Makao Makuu ya WHO, Prof. Teri Reynolds, alisema nchi hizo zimechaguliwa kutokana na uwekezaji wao katika mifumo ya huduma za dharura kwa zaidi ya miaka 10.

Alisema zimejenga msingi imara, ingawa huduma hizo bado hazijafika maeneo yote kwa kiwango kinachohitajika.

Prof. Reynolds alipinga dhana kwamba huduma za dharura ni ghali na si za lazima, akisema ni miongoni mwa huduma za afya zenye gharama nafuu ikilinganishwa na manufaa yake katika kuokoa maisha.

Alisema huduma hizo zina ufanisi mkubwa wa gharama zikilinganishwa na huduma nyingine za msingi, ikiwemo udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza na afya ya uzazi.

Kwa mujibu wa WHO, tafiti katika nchi mbalimbali za Afrika na Asia zinaonyesha mchango mkubwa wa huduma bora za dharura katika kuokoa maisha.

Uturuki yaahidi dola milioni 280 kukamilisha mradi wa SGR

Tanzania iko mbioni kukamilisha mazungumzo na Benki ya Exim ya Uturuki kupata ufadhili wa dola milioni 280 za Marekani kwa ajili ya ujenzi wa vipande vya tatu na nne vya Reli ya Kisasa (SGR).

Mazungumzo hayo yalifanyika Antalya, Uturuki, pembezoni mwa Mkutano wa 31 wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP31), kati ya Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar, na Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Ali Guney.

Balozi Omar alisema vipande hivyo, vyenye urefu wa zaidi ya kilometa 700, vinakadiriwa kugharimu dola bilioni 1.6. Kati ya fedha hizo, dola bilioni 1.32 zimepatikana, huku milioni 280 zikihitajika kukamilisha ufadhili.

Alisema SGR, yenye urefu wa zaidi ya kilometa 2,000, inalenga kuunganisha Bandari ya Dar es Salaam na Mwanza, Kigoma na nchi jirani za Rwanda, Uganda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Mradi huo una sehemu sita, ambapo mbili za mwanzo, kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma, zimekamilika na kuanza kutoa huduma zilizopokelewa vizuri na wananchi.

Balozi Omar alisema tofauti na reli nyingi za kikanda zinazotumia dizeli, SGR ya Tanzania inaendeshwa kwa umeme, hivyo kusaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira na kuunga mkono ajenda ya nishati safi iliyosisitizwa COP31.

Kwa upande wake, Guney alisema benki yake inatambua umuhimu wa SGR kwa Tanzania na nchi jirani, huku ikiangalia fursa nyingine za ufadhili katika uchumi, biashara na miundombinu, ikiwemo barabara na madaraja.

Alisema ushirikiano huo unaendana na azma ya Rais Samia Suluhu Hassan na Rais Recep Tayyip Erdogan kuongeza biashara kati ya Tanzania na Uturuki hadi angalau dola bilioni moja za Marekani.



Mwinyi aeleza fursa mpya za ushirikiano na Oman

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema ziara ya Waziri wa Mambo ya Kale na Utalii wa Oman, Sayyid Ibrahim bin Said Al Busaidi, ni ishara ya dhamira ya kuimarisha uhusiano wa kihistoria na ushirikiano wa muda mrefu kati ya Zanzibar na Oman.

Amesema uhusiano huo una mizizi ya kihistoria na unapaswa kuendelezwa kupitia ushirikiano wenye tija katika sekta mbalimbali, hususan utalii, uhifadhi wa urithi wa kihistoria na uwekezaji.

Dkt. Mwinyi aliyasema hayo Novemba 13, 2026, alipokutana na Waziri Al Busaidi katika mazungumzo yaliyofanyika Ikulu Zanzibar, ambapo alisisitiza umuhimu wa kutekeleza kwa vitendo Hati ya Makubaliano (MoU) iliyosainiwa kati ya pande hizo.

Alisema makubaliano hayo yanaweka msingi wa kuimarisha ushirikiano katika kukuza utalii, kuhifadhi na kuendeleza maeneo ya kihistoria, kuvutia uwekezaji pamoja na kubadilishana uzoefu na utaalamu.

Alifafanua kuwa utekelezaji wa MoU hiyo utaiwezesha Zanzibar kupanua wigo wa kutangaza vivutio vyake vya utalii katika masoko ya kimataifa, hatua inayoweza kuongeza idadi ya watalii na kukuza mchango wa sekta hiyo katika uchumi.

Aidha, alisema ushirikiano huo utatoa fursa ya kutafuta masoko mapya ya utalii, kukarabati na kuendeleza maeneo yenye umuhimu wa kihistoria pamoja na makumbusho yanayohifadhi kumbukumbu za urithi wa Zanzibar.

Dkt. Mwinyi alibainisha kuwa matumizi ya teknolojia za kidijitali katika kuhifadhi urithi wa kihistoria ni eneo jingine muhimu linaloweza kunufaisha pande hizo, likiambatana na kufanya tafiti na kubadilishana utaalamu katika usimamizi wa maeneo ya kihistoria.

Alisema hatua hizo zitasaidia kuhakikisha urithi wa kihistoria unatunzwa na kuendelezwa kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo, huku ukiendelea kuwa sehemu muhimu ya utambulisho wa Zanzibar na kivutio kwa wageni kutoka sehemu mbalimbali duniani.

Kwa upande wake, Waziri Al Busaidi alisema Oman iko tayari kuendeleza na kuimarisha ushirikiano na Zanzibar katika sekta za utalii na urithi wa kihistoria.

Alisema uhusiano wa muda mrefu uliopo kati ya Oman na Zanzibar ni msingi muhimu wa kuendeleza ushirikiano huo, akisisitiza utayari wa nchi yake kushirikiana katika maeneo yaliyokubaliwa. Alieleza kuwa ushirikiano huo una nafasi ya kufungua fursa mpya za maendeleo, hususan katika uhifadhi wa historia na kukuza utalii, sekta zinazoweza kuimarisha zaidi uhusiano wa wananchi wa pande hizo mbili.



HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU NA

Na Ukhti Fatima SS
0789 201 383



Uchumi wa Halal si mpango wa kueneza dini

LAGOS, NIGERIA: Uchumi wa Halal si mpango wa kueneza dini ya Kiislamu, bali ni fursa ya biashara inayozingatia ubora, usafi na uzalishaji wenye maadili, amesema Balozi wa Malaysia nchini Nigeria, Aiyub Omar.

Akizungumza baada ya kutembelea Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Lagos, Aiyub amesema uchumi wa Halal umekuwa sekta muhimu ya kimataifa inayotoa fursa kwa watu wa dini mbalimbali.

Alisema soko hilo, lenye thamani inayokadiriwa kufikia dola trilioni 3.5 za Marekani, linajumuisha vyakula, dawa, vipodozi, fedha za Kiislamu, usafirishaji na utalii.

Balozi huyo alisema Nigeria ina nafasi kubwa ya kunufaika na soko hilo kutokana na rasilimali zake za kilimo, idadi kubwa ya watu na shughuli za ujasiriamali.

Alieleza kuwa Malaysia iko tayari kuisaidia Nigeria kuimarisha mfumo wa uthibitishaji wa bidhaa za Halal, kuboresha viwango vya uzalishaji na kupanua masoko ya kimataifa.

Hatua hizo zinalenga kuongeza thamani ya mazao kama kakao, mawese na tangawizi pamoja na bidhaa za mifugo.

Aiyub alisema hata nchi zisizo na Waislamu wengi zinashiriki katika biashara ya Halal kutokana na fursa zake za kiuchumi.

Kwa mujibu wake, mauzo ya bidhaa za Halal za Malaysia nje ya nchi yalifikia dola bilioni 16.9 mwaka 2025, ongezeko la asilimia 10.9.

Benki ya Kiislamu kufadhili reli kati ya Asia na Ulaya

Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB) na Serikali ya Uturuki zimesaini makubaliano ya ufadhili wa euro milioni 660 kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Istanbul North Rail Crossing, inayolenga kuimarisha usafirishaji wa mizigo na abiria kati ya Asia na Ulaya.

Makubaliano hayo yamesainiwa mwanzoni mwa wiki hii, katika Mkutano wa 31 wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP31), unaofanyika Antalya, Uturuki.

Mradi huo unatarajiwa kujumuisha takribani kilomita 127 za reli inayotumia umeme, pamoja na mifumo ya kisasa ya kuongoza treni, ili kuongeza ufanisi wa biashara na kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Kwa mujibu wa IsDB, makubaliano hayo ni makubwa zaidi kuwahi kufanywa na benki hiyo katika ufadhili wa serikali ya Uturuki, huku jumla ya mikataba 10 yenye thamani ya dola bilioni 5.1 ikitangazwa katika hafla hiyo kwa ushirikiano wa taasisi mbalimbali za kifedha.

Hatua hiyo inaonesha kuongezeka kwa nafasi ya taasisi za kifedha za Kiislamu katika kugharamia miundombinu mikubwa ya kimataifa inayochochea biashara, uchumi na maendeleo endelevu.

Vyanzo: Vyanzo mbalimbali

Vyeti vya Halal Indonesia lazima kwa bidhaa ifikapo 2028

JAKARTA, INDONESIA: Serikali ya Indonesia inaongeza maandalizi ya kutekeleza kikamilifu masharti ya lazima ya uthibitishaji wa Halal kwa makundi mbalimbali ya bidhaa ifikapo Oktoba 17, 2028.

Kwa mujibu wa Kanuni ya Serikali Namba 40 ya mwaka 2026, muda wa utekelezaji umeongezwa kwa baadhi ya bidhaa, zikiwemo vyakula na vinywaji vinavyozalishwa na wafanyabiashara wadogo, vipodozi, bidhaa fulani zinazoagizwa kutoka nje na bidhaa nyingine za matumizi ya kila siku.

Naibu Mratibu wa Uimarishaji wa Utambulisho wa Taifa, Warsito, amesema serikali inaandaa mpango wa utekelezaji kwa kushirikisha wizara, taasisi na serikali za maeneo mbalimbali.

Amesema uthibitishaji wa Halal si suala la kutimiza masharti ya kisheria pekee, bali pia kuhakikisha usalama na uhakika kwa watumiaji na kuongeza ushindani wa bidhaa za ndani.

Katika maandalizi hayo, serikali itaweka mkazo katika kuwasaidia wafanyabiashara wadogo kupata vyeti, kuongeza huduma za ukaguzi na kuimarisha ufuatiliaji wa malighafi na bidhaa zinazoagizwa kutoka nje.

Warsito amesisitiza kuwa kipindi cha 2026 hadi 2028 kinapaswa kutumika kuimarisha utayari wa wafanyabiashara badala ya kuchelewesha maandalizi.

Hadi Novemba 2026, zaidi ya bidhaa milioni 15.4 zilikuwa zimepata uthibitisho wa Halal nchini Indonesia.

Mauritius kuandaa tuzo za fedha za Kiislamu Afrika

MAURITIUS: Nchi ya Mauritius inatarajiwa kuwa mwenyeji wa hafla ya 12 ya Tuzo za Fedha za Kiislamu Afrika, itakayofanyika Desemba 1, 2026, katika hoteli ya Holiday Inn Mauritius Mon Trésor.

Tuzo hizo, zinazoandaliwa na Kituo cha AlHuda cha Benki na Uchumi wa Kiislamu (AlHuda CIBE), zinalenga kutambua taasisi na wataalamu waliochangia maendeleo ya huduma za fedha za Kiislamu barani Afrika.

Kwa mujibu wa waandaaji, tuzo zitatolewa katika maeneo mbalimbali, yakiwemo benki za Kiislamu, bima ya Takaful na Re-Takaful, hati fungani za Sukuk, huduma ndogo za fedha na teknolojia za kifedha zinazozingatia Sharia.

Hafla hiyo itaambatana na Mkutano wa 12 wa Fedha za Kiislamu Afrika, utakaofanyika Desemba 1 hadi 3, ukikutanisha taasisi za fedha, wasimamizi wa sekta, wawekezaji na wanazuoni wa Sharia.

BAYTULMAAL TANZANIA
TAMPRO
"Takasa Mali Jenga Matumaini"

زكاة

NA
Baitulmaal Tanzania

JUKWAA LA ZAKA

Historia ya usimamizi wa Zaka na maendeleo ya Baytulmaal

SEHEMU YA
3

Umar bin Abdul Aziz na mageuzi katika usimamizi wa Baytulmaal

Miongoni mwa vipindi vinavyotajwa sana kama mfano wa ufanisi na mafanikio katika historia ya usimamizi wa Baytulmaal ni kipindi cha Khalifa Umar bin Abdul Aziz (Allah amrehemu), aliyeongoza dola ya Kiislamu ya Banu Umayyah kuanzia mwaka 99 hadi 101 Hijria, sawa na takribani mwaka 717 hadi 720 Miladia.

Licha ya kutawala kwa muda mfupi, Umar bin Abdul Aziz anakumbukwa kwa juhudi zake za kurejesha uadilifu, kupambana na matumizi mabaya ya mali za umma, kuimarisha ukusanyaji na ugawaji wa zaka, kurekebisha mfumo wa kodi na kusimamia haki za wananchi.

Mafanikio yanayohusishwa na utawala wake hayakutokana na jambo moja pekee, bali mabadiliko katika ukusanyaji wa mapato, udhibiti wa matumizi, usimamizi wa mali na kuhakikisha rasilimali za umma zinawanufaisha wanaostahili.

Hali ya Baytulmaal kabla ya mageuzi yake

Mfumo wa Baytulmaal ulianza katika zama za Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) na kuimarishwa katika vipindi vya Makhalifa wanne waongofu. Mfumo huo uliendelea chini ya tawala mbalimbali za Kiislamu, ikiwemo dola ya Banu Umayyah, ambako Umar bin Abdul Aziz alikuja kufanya mageuzi makubwa katika usimamizi wake

Katika vipindi vyote hivyo, kadri dola ya Kiislamu ilivyopanuka, mapato ya Serikali yaliongezeka, lakini pia majukumu yake yakawa makubwa zaidi.

Katika baadhi ya vipindi vya utawala wa Banu Umayyah, changamoto zilijitokeza za matumizi mabaya ya rasilimali za umma, upendeleo na malalamiko kuhusu ukusanyaji wa kodi.

Hivyo, Umar bin Abdul Aziz alipoingia madarakani, alianza harakati za kuleta mageuzi kwa kurekebisha mfumo uliokuwepo, kuimarisha uadilifu na kurejesha imani ya wananchi katika utawala.

Kurejesha uadilifu katika usimamizi wa mali za umma

Msingi muhimu wa mageuzi yake ulikuwa kutambua kwamba mali za umma ni amana, si mali binafsi ya mtawala au familia yake. Alijitahidi kuzuia matumizi ya rasilimali za Serikali kwa manufaa binafsi yasiyo ya haki, kupunguza ubadhirifu na kupambana na upendeleo katika ugawaji wa mali.

Msimamo huo unaendana na kauli ya Mwenyezi Mungu: “Kwa hakika, Allah anakuamrisheni kuzirudisha amana kwa wenyewe.” [Qur’an, 4:58]

Katika Al-Muwatta ya Imam Malik, kuna riwaya inayomhusisha Umar bin Abdul Aziz na maagizo ya kurejesha mali zilizochukuliwa kwa dhuluma kwa wenyewe, huku suala la zaka likishughulikiwa kwa kuzingatia hukumu husika.

Hatua hii ilikuwa na maana kubwa katika usimamizi wa Baytulmaal. Ilisisitiza kwamba kuimarisha hazina ya umma hakumaanishi kukusanya fedha nyingi kwa njia yoyote, bali kuhakikisha mali inapatikana na kutumika kwa njia halali.

Kuimarisha ukusanyaji na ugawaji wa zaka

Zaka ilikuwa miongoni mwa maeneo muhimu katika sera za kifedha za Umar bin Abdul Aziz.

Alisisitiza ukusanyaji wake kwa mujibu wa Sharia na kuhakikisha mapato yanawafikia watu wenye haki ya kuyapokea.

Qur’an inataja makundi manane ya wanaostahili zaka: “Wa kupewa sadaka ni mafakiri, na masikini, na wanao zitumikia, na wa kutiwa nguvu nyoyo zao, na katika kukomboa watumwa, na wenye madeni, na katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na wasafiri. Huu ni waajibu ulio faridhiwa na Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima.” [Qur’an, 9:60].

Katika mfumo huu, zaka si sadaka ya hiari inayotolewa kwa hisani ya mtawala, bali ni wajibu wa kidini wenye masharti na wapokeaji maalumu. Mageuzi ya Umar yalisisitiza umuhimu wa kutambua wahitaji, kusimamia makusanyo na kuhakikisha ugawaji unazingatia haki badala ya upendeleo.

Katika baadhi ya simulizi za kihistoria, mafanikio ya usimamizi huo yanahusishwa na hali ya wasimamizi wa zaka kukosa wapokeaji katika maeneo fulani baada ya kuwasaidia wahitaji waliotambuliwa.

Hata hivyo, simulizi hizo hazitoshi kuthibitisha kwamba umaskini ulitoweka kabisa katika dola yake yote.

Kurekebisha kodi na kuondoa dhuluma

Mageuzi mengine muhimu yalihusu ukusanyaji wa kodi na mapato mengine ya Serikali.

Mbali na zaka, Baytulmaal ilipata mapato kupitia kharaj, yaani mapato ya ardhi, na jizyah, ushuru uliowekwa kwa wasiokuwa Waislamu chini ya utawala wa Kiislamu kwa masharti husika.

Umar alijitahidi kurekebisha mfumo huo ili kuzuia dhuluma na kuhakikisha wananchi hawatozwi kodi kinyume na haki zao.

Mojawapo ya hatua zinazotajwa katika historia yake ni kuagiza kwamba watu walioingia katika Uislamu wasiendelea kulazimishwa kulipa jizyah kwa sababu ya hali yao ya awali.

Katika baadhi ya maeneo, watendaji wa Serikali walilalamika kwamba mapato ya jizyah yalikuwa yakipungua kutokana na watu wengi kuingia katika Uislamu.

Umar alisisitiza kwamba jukumu la Mtume (Allah amshushie rehema na amanu) lilikuwa kuwaongoza watu, si kuifanya dini kuwa chombo cha kukusanya kodi.

Msimamo huo ulionyesha kwamba Serikali haikupaswa kutanguliza mapato ya kifedha kuliko haki za kidini za wananchi.

٧ جمادى الآخرة ١٤٤٨هـ

HABARI KIMATAIFA

NA
Na Mugini Singira
0786 630 345



Waingereza 78% wanaamini Israel tishio kwa amani ya dunia

LONDON, UINGEREZA: Asilimia 78 ya wananchi wa Uingereza wanaiona Israel kuwa tishio kubwa kwa amani duniani, ikilinganishwa na asilimia 48 mwaka 2005, kwa mujibu wa utafiti mpya uliochapishwa Novemba 2026.

Utafiti huo wa Kituo cha Taifa cha Utafiti wa Kijamii (NatCen), uliofanyika katika majira ya kuchipua mwaka 2026, unaonyesha kuongezeka kwa wasiwasi kuhusu Israel, hasa kufuatia vita vya Gaza na kuongezeka kwa migogoro Mashariki ya Kati.

Mwaka 2024, asilimia 73 ya Waingereza waliona Israel kuwa tishio kubwa, kabla ya kiwango hicho kufikia asilimia 78 mwaka huu.

Kwa kulinganisha, asilimia 75 wanaiona Iran kuwa tishio, Marekani asilimia 74 na China asilimia 62. Urusi inaongoza kwa asilimia 89.

Mitazamo pia inatofautiana kisiasa. Asilimia 88 ya wafuasi wa chama cha Green wanaiona Israel kuwa tishio, ikilinganishwa na asilimia 84 ya Labour, 70 ya Conservative na 62 ya Reform UK. Mwandishi wa ripoti hiyo, Sophia Gaston, amesema sifa ya Israel imeathiriwa na ushiriki wake katika migogoro ya Mashariki ya Kati.

Watafiti wanaeleza kuwa wasiwasi huo unaweza pia kuchangiwa na hofu ya vita hivyo kusambaa katika eneo kubwa zaidi.

Familia 46,000 zaathiriwa na mafuriko, maelfu wakosa makazi

Takribani familia 46,000, zinazojumuisha watu 226,000 zimeathiriwa na mafuriko Ukanda wa Gaza, Palestina, kufuatia mvua kubwa zilizoanza Novemba 6, 2026.

Mvua hizo zmezidisha hali ngumu ya maisha ya Wapalestina waliokimbia makazi yao kutokana na vita.

Kwa mujibu wa ripoti ya Umoja wa Mataifa iliyotolewa mwishoni mwa wiki hii, zaidi ya makazi 40,000 ya muda yameripotiwa kuharibika, yakiwemo zaidi ya 9,000 ambayo huenda hayawezi kutumika tena. Aidha, takribani wanafunzi 5,500 wameshindwa kuendelea na masomo baada ya vituo 109 vya kujifunzia kuathiriwa na mafuriko hayo.

Hali hiyo imeongeza hatari ya kusambaa kwa magonjwa kutokana na maji ya mvua kuchanganyika na majitaka, huku baadhi ya vituo vya afya vikisitisha huduma.

Watu 333,000 Yemen wakimbia makazi ndani ya miezi 3

Zaidi ya watu 333,000 wamelazimika kukimbia makazi yao katika maeneo ya magharibi mwa Yemen kati ya Agosti 1 na Novemba 10, 2026, kutokana na kuongezeka kwa mapigano, huku maelfu ya familia zikihitaji msaada wa dharura.

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) iliyotolewa Wiki hii, jumla ya watu 333,125 kutoka familia 55,514 wamehama katika kipindi hicho.

Jimbo la Taiz limepokea watu 141,096, sawa na asilimia 42 ya waliohama, likifuatiwa na Lahj lenye watu 84,714 na Aden yenye watu 66,792.

Ongezeko hilo limeweka shinikizo kubwa kwa jamii zinazowapokea wakimbizi wa ndani, hususan katika upatikanaji wa chakula, maji safi, makazi na huduma za afya.

Hali hiyo inazidisha mgogoro wa kibinadamu nchini Yemen, ambako mapigano ya muda mrefu yameathiri maisha ya mamilioni ya wananchi na kudhoofisha juhudi za kurejesha amani na shughuli za kiuchumi.

Wanafunzi Waislamu Uphilipino wataka haki ya kuvaa hijab chuoni

Wanafunzi Waislamu na viongozi wa jamii nchini Uphilipino wameitaka Iligan Medical Center College kuheshimu haki ya wanafunzi wa kike kuvaa hijab wakati wa masomo na mafunzo ya uuguzi, kufuatia malalamiko yaliyowasilishwa katika Tume ya Elimu ya Juu Novemba 4, 2026.

Mvutano huo umeripotiwa tena Novemba 10, huku uongozi wa chuo ukikanusha kuwapo kwa marufuku ya jumla ya hijab na kuahidi kupitia kanuni za sare. Suala hilo limeibua mjadala kuhusu uhuru wa dini na haki ya kupata elimu bila ubaguzi.

Vyanzo: Vyanzo mbalimbali

٧ جمادى الآخرة ١٤٤٨هـ

DARASA LA WIKI



SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811

Athari za kusengenya kidini na kijamii

Miongoni mwa magonjwa ya kijamii yanayosababishwa na matumizi mabaya ya ulimi, ambayo yamekithiri katika mazingira yetu nyumbani, kwenye vikao au katika mikusanyiko mbalimbali, ni tabia ya kusengenya. Kwa hakika, watu wengi wameshindwa kujiepusha na tabia hiyo, isipokuwa wale ambao Mwenyezi Mungu amewakinga dhidi ya maovu hayo. Licha ya kuzoeleka kwake katika jamii, tabia hii ina madhara makubwa kwa dini na jamii kwa ujumla. Uislamu, ambao ni mfumo kamili wa maisha ya mwanadamu umekuja kulinda dini, nafsi, mali, akili na heshima ya mwanadamu. Kwa hiyo, kusengenya ni kuvamia moja kwa moja heshima na hadhi ya Muislamu.

Maana ya kusengenya

Kusengenya ni kumtaja mwenzako kwa jambo ambalo hapendi litajwe kuhusu yeye. Mtume (rehema na amani za Allah ziwe juu yake) amefafanua maana ya kusengenya pale alipowauliza Maswahaba wake: “Je, mnajua kusengenya ni nini?”Maswahaba wakajibu: “ Allah na Mtume wake wanajua zaidi.”

Mtume akasema: “Ni kumtaja ndugu yako kwa jambo asilolipenda.” Maswahaba wakamuuliza: “Unaonaje ikiwa jambo ninalolisema kuhusu ndugu yangu analo?” Akajibu: “Ikiwa jambo unalolisema analo kweli, basi utakuwa umemsengenya. Na ikiwa jambo hilo hana, basi umemzulia uongo.” [Muslim].

Kusengenya ni haramu kwa mujibu wa Qur’an na hadith. Allah Mtukufu amefananisha kusengenya na jambo ovu aliposema: “Enyi mliyoamini! Jiepusheni na dhana, kwani hakika baadhi ya dhana ni dhambi. Na wala msichunguzane, na wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi. Je, yupo katika nyinyi anayependa kula nyama ya nduguye aliyekufa? Mmelichukia hilo...!” [Qur’an, 49:12].

Ni mfano wa kutisha ulioje! Mtu kula nyama ya nduguye aliyefariki! Mfano huu unaonesha ubaya na uzito wa kitendo hicho. Mwanazuoni Hasan al–Basri (Allah amrehemu) ameeleza kuwa kumzungumzia mtu mwingine kunaweza kugawanywa katika aina tatu:

Kwanza, kusengenya (ghiba). Huku ni kumtaja ndugu yako kwa jambo ambalo kweli analo, lakini hapendi lisemwe au lijadiliwe mbele ya watu. Pili, kumzulia uongo (buhtan). Huku ni kumhusisha ndugu yako na jambo ambalo hana, kwa maana ya kumpa tuhuma za uongo.

Tatu, kuzua au kusambaza habari za uongo (ifk). Huku ni kupokea habari zinazomhusu mtu mwingine na kuzisambaza bila kuhakikisha ukweli wake.

Ikumbukwe kuwa kusengenya kunaweza kufanyika kwa njia mbalimbali, kama vile kumdharau mtu kwa ishara, kumsema, kumkejeli, kumwandikia au kuandika habari zinazomchafua.

Zamani, kusengenya kulikuwa kunaishia katika mipaka ya kikao kimoja. Lakini leo hii, kunaweza kusambaa ndani ya dakika chache

na kuwafikia maelfu ya watu kupitia kioo kidogo cha simu. Mitandao ya kijamii imekuwa mlango mpana wa kueneza tabia ya kusengenya.

Ni maoni mangapi ya kejeli yanayotolewa, picha ngapi zinazosambazwa na video ngapi zinazochapishwa katika makundi ya faragha, ambayo yote hutumika kumdhalilisha mtu, kufichua upungufu wake au kumfanya aonekane kichekesho mbele ya jamii?

Sababu za kusengenya

Miongoni mwa sababu zinazochangia tabia ya kusengenya ni udhaifu wa imani. Vilevile, husuda inaweza kumfanya mtu kumsema vibaya mwenzake kutokana na chuki au kutopenda kuona neema alizojaliwa. Mtu anaweza kumsengenya mwingine kwa sababu ya kushindania cheo, umaarufu, mali au nafasi katika jamii.

Wanazuoni wameeleza kuwa kuna baadhi ya mazingira ambayo kumtaja mtu kwa jambo asilolipenda hakuchukuliwi kuwa ni kusengenya kulikoharamishwa katika Uislamu.

Miongoni mwa mazingira hayo ni: Kwanza, kuwasilisha malalamiko mbele ya mahakama au mamlaka husika. Katika mazingira haya, mtu anayeripoti dhuluma aliyofanyiwa anaruhusiwa kueleza yaliyomtokea, hata kama kufanya hivyo kutahusisha kumtaja mtu aliyemdhulumu.

Allah anasema: “Mwenyezi Mungu hapendi maovu yatangazwe hadharani, isipokuwa kwa yule aliyedhulumiwa.” [Qur’an, 4:148].

Pili, mtu anayetangaza uzushi au maasi yake hadharani. Mtu wa aina hii anaweza kutajwa kwa matendo yake hayo ili kuwaonya watu na kuwakinga dhidi ya madhara yanayoweza kusababishwa na vitendo vyake.

Tatu, kuomba fat–wa kuhusu jambo maalumu linalomhusu mtu, kwa lengo la kupata ufafanuzi wa hukumu ya kisharia. Mfano wa hili ni tukio la Hind, mke wa Abu Sufyan, alipomuuliza Mtume wa Allah kuhusu mume wake.

Hind alisema: “Abu Sufyan ni mtu mchoyo, hanipi matumizi yanayonitosheleza mimi na mwanangu.” Mtume akamwambia: “Chukua kiasi kinachokutosha wewe na mwanao kwa namna inayokubalika.”

Nne, kuulizia hali ya mtu anayetaka kuoa. Mfano wa jambo hili ni tukio la Fatima binti Qais, ambaye alimuuliza Mtume kuhusu baadhi ya wanaume waliokuwa wamekuja kumposa ili apate ufafanuzi kuhusu hali zao.

Mtume akamwambia: “Abu Jahm haweki fimbo yake begani mwake (kwa maana, ana tabia ya kumpiga mwanamke), na Muawiya ni mtu masikini asiye na mali. Olewa na Usamah bin Zaid.”

Njia za kujiepusha

Namna ya kujikinga na usengenyi na kujitibu na tabia hii ovu ni kumcha Allah, kushughulika na upungufu wako mwenyewe, kujihesabu na kujitathmini, kudumu katika kumtaja Allah, kuleta nyiradi mbalimbali na kukaa nyumbani isipokuwa panapokuwa na haja ya kutoka.

Kafara (fidia) ya kusengenya ni kumjulisha mtu uliyemsengenya kuhusu maneno uliyoyasema dhidi yake au vitendo ulivyovifanya vinavyomhusu. Aidha, mtu anatakiwa kutubu kwa Allah Mtukufu, kutoa nasaha na mawaidha kwa wengine, na kujiepusha na tabia hiyo mbaya.

NA UKHTI FATIMA



Mbinu 3 rahisi za kuendesha kampeni ya kuongeza mauzo

Unaweza kuwa na bidhaa nzuri, bei nzuri na huduma nzuri, lakini wateja wasinunue kama unavyotarajia. Wengine wanaingia dukani, wanauliza bei na kuondoka. Wengine wanaahidi kurudi, lakini hawaonekani tena. Wapo pia wateja wa zamani ambao wameacha kununua kwako.

Katika hali kama hii, si lazima upunguze bei za bidhaa zote au utumie fedha nyingi kutangaza biashara yako. Wakati mwingine unahitaji tu kutoa sababu nzuri itakayomshawishi mteja kununua sasa badala ya kuendelea kusubiri.

Hapo ndipo umuhimu wa kufanya kampeni maalumu ya kuongeza mauzo unapojitokeza.

Kampeni hiyo inaweza kuwa punguzo la bei kwa muda maalumu, zawadi ndogo kwa mnunuzi, fursa ya kujaribu bidhaa au huduma nyingine inayompa mteja manufaa ya ziada. Lakini kampeni si kupunguza bei tu. Ili ifanikiwe, inahitaji maandalizi. Mambo matatu yafuatayo yanaweza kumsaidia hata mfanyabiashara mwenye mtaji mdogo.

Kwanza, tambua unataka kumvutia nani

Kosa ambalo wafanyabiashara wanaweza kufanya ni kuanzisha kampeni bila kujua hasa wanataka kufanikisha nini.

Jiulize: Unataka kupata wateja wapya? Unataka wateja wa zamani warudi? Unataka wanaonunua bidhaa moja waanze kununua nyingine? Au unataka kuongeza mauzo katika siku ambazo biashara huwa ndogo?

Majibu ya maswali hayo yatakuonyesha kampeni inayokufaa.

Kwa mfano, ikiwa una duka la nguo na unataka kuwavutia wateja wapya, unaweza kutoa punguzo maalumu kwa wanaonunua kwa mara ya kwanza. Ikiwa una mgahawa ambao huwa na wateja wachache wakati fulani, unaweza kuandaa ofa ya chakula katika saa hizo.

Na kama una wateja ambao wamekaa muda mrefu bila kurudi, unaweza kuwatumia ujumbe wa kuwajulisha bidhaa mpya au ofa iliyopo.

Muhimu ni kutaka kutatua tatizo moja kwa wakati. Kampeni moja haiwezi lazima kukuletea wateja wapya, kuwarudisha wa zamani na kuongeza mauzo ya bidhaa zote kwa wakati mmoja.

Pili, mpe mteja sababu ya kununua

Baada ya kutambua wateja unaowalenga, hatua inayofuata ni kuandaa kitu kitakachowavutia.

Njia mojawapo ni punguzo la bei. Kwa mfano, unaweza kupunguza bei ya bidhaa fulani kwa siku tatu au kutoa punguzo kwa mteja anayenunua bidhaa nyingi.

Lakini kuwa mwangalifu. Punguzo kubwa linaweza kuvutia wanunuzi wengi huku likikuacha na hasara. Kabla ya kuamua, hesabu gharama ya bidhaa, bei utakayouzia na faida itakayobaki.

Njia nyingine ni kumpa mteja nafasi ya kujaribu bidhaa kabla ya kununua.

Mfano, ikiwa unauza juisi mpya, unaweza kuwapa wateja kiasi kidogo waonje. Anayeuza manukato anaweza kuwaruhusu wateja kujaribu harufu. Mtoa huduma naye anaweza kutoa huduma ndogo ya majaribio.

Lengo ni kumwezesha mteja kufahamu ubora wa unachouza bila kulazimika kutumia fedha nyingi kabla ya kukiamini.

Unaweza pia kutoa zawadi ndogo kwa wanunuzi au kuandaa siku maalumu ya kutambulisha bidhaa mpya. Hata hivyo, usitoe ofa kwa sababu tu wafanyabiashara wengine wanafanya hivyo. Chagua njia inayolingana na uwezo wako na mahitaji ya wateja.

Tangazo lako liwe rahisi kueleweka. Eleza bidhaa, manufaa, bei, muda wa ofa na mahali pa kuipata.

Ikiwa ofa inaisha Jumamosi, sema hivyo wazi. Usidai muda unakaribia kuisha ikiwa si kweli.

Tatu, pima kama kampeni imeleta faida

Wafanyabiashara wengine hupima mafanikio kwa kuona wateja wengi wameingia dukani. Lakini wingi wa wateja pekee hautoshi.

Jiulize: Mauzo yameongezeka kwa kiasi gani? Umepata wateja wangapi wapya? Wateja wa zamani wamerudi? Na baada ya kutoa punguzo au zawadi, faida imebakia kiasi gani?

Kwa mfano, kabla ya kampeni unaweza kuwa ulikuwa unauza bidhaa 10 kwa siku. Baada ya kampeni, ukauza 20. Hiyo ni hatua nzuri, lakini bado unapaswa kuangalia gharama ulizotumia na faida halisi.

Si lazima uwe na kompyuta au programu ghali kufanya tathmini hiyo. Daftari la kawaida linaweza kukusaidia kurekodi mauzo kabla, wakati na baada ya kampeni.

Kama kampeni haijafanikiwa, chunguza sababu. Huenda ofa haikuwavutia wateja, tangazo halikuwafikia watu unaowalenga au muda haukuwa mzuri.

Usikate tamaa. Rekebisha pale ulipokosea na ujaribu tena.

Kumbuka, lengo la kampeni ya mauzo si kufanya biashara ionekane ina wateja wengi kwa siku chache. Ni kuongeza mauzo kwa njia inayokuletea faida na kujenga uhusiano mzuri na wateja.

Kwa hiyo, kabla ya kutoa punguzo au zawadi, jiulize mambo matatu: Ninataka kumvutia nani? Nitampa sababu gani ya kununua? Nitajuaje kama nimefanikiwa?

Majibu hayo yanaweza kukusaidia kutumia vizuri hata fedha kidogo ulizonazo kukuza biashara yako.

NA
Abeid Othman
0754 990 083

Tabia zetu Waislamu zinawavutia wengine kwenye dini?

Uislamu ni dini ya vitendo na mwanga unaoangazia njia ya mwanadamu. Katika ulimwengu wa leo uliojaa changamoto nyingi za kimaadili, silaha kubwa na bora zaidi ya kueneza ujumbe wa Mwenyezi Mungu si hotuba ndefu wala malumbano, bali ni akhlaq (tabia njema).

Tabia zetu kama Waislamu zinapaswa kuwa kielelezo na kivutio tosha kinachowafanya wasiokuwa Waislamu kutamani Uislamu na hatimaye kuamua kusilimu kwa hiari yao wenyewe.

Tukirudi kwenye historia ya mwanzo wa Uislamu, mafanikio makubwa ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) hayakujengwa juu ya nguvu ya upanga au mabavu, bali yalijengwa juu ya nguzo kuu ya akhlaq tukufu. Mtume alikuwa ni mfano hai wa Qur'an inayotembea.

Kabla hata hajateuliwa kuwa Mtume, jamii ya Kikuraishi ilimpa jina la Al-Amin (mwaminifu) na As-Sadiq (mkweli). Tabia yake njema, uaminifu wake, uvumilivu wake kwa watesi wake, na upole wake kwa wadogo na wakubwa, vilimfanya awe kipenzi cha wengi.

Hata maadui zake wakubwa walipomkimbia, walifanya hivyo kwa sababu ya hofu ya ujumbe wake, lakini mioyoni mwao walikuwa wakimkubali na hata kuweka amana zao kwake.

Watu wengi waliingia kwenye Uislamu sio kwa sababu walifanya mijadala mirefu ya kidini, bali walivutwa na tabia yake isiyo na dosari.

Alikuwa akiwatendea wema hata wale waliomfanyia ukatili. Huu ndio mtindo wa ulinganizi unaotakiwa, yaani kuongoza kwa vitendo na si kwa maneno matupu.

Majirani kipimo cha Uislamu wetu

Uislamu umetilia mkazo mkubwa suala la jirani. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) aliwahi kusema kuwa Jibril (Amani imshukie) alikuwa akimhusia kuhusu jirani mara kwa mara mpaka akadhani angewarithisha.

Hii inaonyesha kuwa uhusiano na jirani ndiyo picha ya kwanza na ya wazi kabisa inayompa mtu taswira ya Uislamu ulivyo.

Kama tunaishi na majirani zetu wasio Waislamu au Waislamu wenzetu kwa njia ya wema, upendo, na msaada, tunakuwa mabalozi wazuri wa dini yetu. Jirani anapomuona Muislamu ni mpole, mwenye kujali, anayetoa msaada wakati wa shida, na mwenye kuheshimu haki za wengine, anapata picha halisi kwamba Uislamu ni dini ya amani na rehema.

Hata hivyo, inasikitisha sana kuona hali halisi ya Waislamu wengi leo. Badala ya kuwa taa inayomulika mitaa wanayoishi, wamegeuka kuwa jamii inayojitenga.

Ni jambo la kusikitisha kushuhudia Waislamu wakiishi na migogoro isiyoisha na majirani zao.

Katika mitaa mingi, hali ya kutosalimiana, kutosaidiana katika shida na raha, au hata kushindwa kuulizana hali imekuwa kawaida.

Waislamu wengi wanaonekana kuwa watu wagumu, wenye sura za kukunja na wasiochangamka.

Hata katika mikusanyiko muhimu ya kijamii au shughuli za maendeleo ya jamii, Waislamu wengi wanajitenga au kushindwa kushiriki ipasavyo.

Wanaonekana kana kwamba wanaishi katika kisiwa cha peke yao, wakijifungia kwenye ulimwengu wao bila kujali yanayoendelea kwa majirani zao.

Tabia hii ya kujitenga sio tu kwamba inavunja mafundisho ya Mtume, bali inatoa picha mbaya na potofu kabisa kuhusu Uislamu. Watu wa nje wanaanza kuichukulia dini yetu kuwa ni ngumu, ya chuki, na isiyojali jamii inayowazunguka.

Huu si Uislamu tuliourithi kutoka kwa Mtume wetu (Allah amshushie rehema na amani).

Uislamu ni tabasamu, ni msaada kwa mwenye shida, ni ukarimu kwa jirani, na ni ushirikiano katika mambo mema. Ni wakati sasa wa Waislamu kujitathmini na kubadilisha mtindo wetu wa maisha mitaani.

Tunapokuwa na tabia njema, tutawafanya majirani zetu na jamii kwa ujumla kupenda kuona dini yetu, na hapo ndipo Uislamu utakapozidi kusambaa kwa wepesi na heshima kubwa. Tabia zetu ziwe ndiyo mawaidha yetu ya kwanza kabla hatujatamka neno lolote la kulingania.



٧ جمادى الآخرة
١٤٤٨هـ

KUTOKA KWA MHARIRI

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
0789 201383

Asanteni Shirkah kwa kutufunza uwekezaji halali

Alhamisi iliyopita, lilifanyika Kongamano la Kwanza la Uwekezaji Halali Tanzania, lililoibua mjadala muhimu kuhusu nafasi ya uwekezaji unaozingatia misingi ya Uislamu katika kujenga uchumi imara, jumuishi na wenye baraka.

Kongamano hilo lililofanyika katika Hoteli ya Hyatt Regency jijini Dar es Salaam, liliandaliwa chini ya kaulimbiu isemayo, "Halal Investing Towards a US$1 Trillion Economy", yaani Uwekezaji Halali kuelekea Uchumi wa Dola Trilioni Moja.

Mada zilizowasilishwa katika kongamano hilo zilijikita katika kujadili mchango wa huduma za fedha za Kiislamu, hususan uwekezaji halali katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050.

Kwa hakika, tuna kila sababu ya kuwapongeza waandaaji wa kongamano hilo, kampuni ya Shirkah Asset Management kwa kushirikiana na Kituo cha Fedha za Kiislamu, Uzingatiaji na Ushauri (CIFCA) pamoja na Taqseem Academy.

Pongezi hizo zinatokana na ukweli kwamba kongamano hilo halikuwa tukio la kawaida la kibiashara, bali lilikuwa jukwaa muhimu la kuelimisha jamii kuhusu dhana ya uwekezaji halali na fursa mbalimbali zilizopo katika sekta ya fedha za Kiislamu.

Aidha, kongamano hilo liliwakumbusha Watanzania kuwa uwekezaji unaweza kuwa na manufaa ya kiuchumi huku ukizingatia maadili na misingi ya dini.

Jambo muhimu tunalopaswa kuelewa ni kwamba Uislamu haukatazi kutafuta mali, kufanya biashara wala kuwekeza. Badala yake, unahimiza kufanya kazi, kuzalisha mali na kushiriki katika shughuli za kiuchumi kwa kuzingatia misingi ya uadilifu na uwazi, huku tukijiepusha na mambo yaliyoharamishwa na Mwenyezi Mungu.

Qur'an yatwambia: "...Mwenyezi Mungu amehalalisha biashara na ameharamisha riba..." [Qur'an, 2:275]. Aya hii inabainisha tofauti kati ya biashara halali na riba, huku ikitufundisha kuwa si kila njia ya kupata faida inakubalika mbele ya Mwenyezi Mungu.

Kwa msingi huo, mwekezaji Muislamu hapaswi kuzingatia kiasi cha faida atakachopata pekee, bali pia anapaswa kuangalia uhalali wa shughuli inayozalisha faida hiyo. Na hapo ndipo umuhimu wa kujifunza uwekezaji halali unapojitokeza.

Katika suala la biashara, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesisitiza umuhimu wa ukweli na uaminifu, akisema: "Mfanyabiashara mkweli na mwaminifu atakuwa pamoja na Manabii, wakweli na mashahidi Siku ya Kiyama." [Tirmidhi].

Hadith hii inatukumbusha kuwa biashara na uwekezaji ni sehemu ya ibada inayoweza kumletea mtu malipo mema kutoka kwa Allah, iwapo itafanywa kwa uaminifu na kwa kuzingatia misingi ya dini.

Katika Uislamu, mali ni neema na amana kutoka kwa Allah. Kwa msingi huo, upatikanaji na matumizi yake yanapaswa kuzingatia misingi ya dini, ikiwamo kujiepusha na riba, kamari, biashara ya pombe na shughuli nyingine zilizokatazwa na Uislamu.

Vilevile, uwekezaji halali unapaswa kuepuka vitendo vya udanganyifu, ulaghai, kuficha taarifa muhimu na kutumia udhaifu wa wengine kwa lengo la kujipatia faida. Kwa hapa nchini, uwekezaji halali unaweza kuchangia upatikanaji wa mitaji na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika kufanikisha malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050.

Hata hivyo, matumizi sahihi ya fursa hizo yanahitaji elimu kwa umma kuhusu mifumo ya uwekezaji halali, faida na changamoto zake, pamoja na namna ya kutambua miradi ya kitapeli inayojificha nyuma ya jina la dini.

Tunatoa wito kwa Serikali kuimarisha mifumo ya kisheria na kisera ili kukuza huduma za fedha za Kiislamu na kuhakikisha zinasimamiwa kwa uwazi na weledi. Aidha, tunashauri makongamano ya aina hii yafanyike angalau mara mbili kwa mwaka ili kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu uwekezaji halali na fursa zilizopo katika sekta hiyo.

Ni muhimu pia elimu kuhusu uwekezaji halali isambazwe katika mikoa mbalimbali nchini, vyuo vikuu, taasisi za elimu na jumuiya za wafanyabiashara ili kuwafikia wananchi wengi zaidi. Mwisho, tunatoa shukrani zetu za dhati kwa Shirkah, CIFCA na Taqseem Academy kwa kutuelimisha na kutukumbusha kuwa mafanikio ya kiuchumi yanapaswa kwenda sambamba na maadili na misingi ya dini.

٧ جمادى الآخرة ١٤٤٨هـ

NASAHA ZA WIKI



NA
Yusufu Amini
0787 503 085

Jinsi ya kupata utulivu katika sala

Kukosa unyenyekevu (khushui) katika sala ni mojawapo ya matatizo makubwa yanayowakabili Waislamu wengi katika zama hizi. Wengi husali bila kutimiza ipasavyo nguzo na masharti ya sala, yakiwamo kutulia katika vitendo vya sala mahali panapohitajika, kuzingatia wanayoyasema na kusali kwa utulivu na umakini.

Umuhimu wa kutimiza nguzo za sala unatokana na ukweli kwamba sala ndiyo ibada ya kwanza kuhesabiwa Siku ya Kiyama. Sala ikiwa nzuri (ikikamilika), amali zilizobakia zitakuwa nzuri; na ikiwa mbaya amali zote zitakuwa mbaya.

Kwa maana nyingine, haitozingatiwa Siku ya Kiyama kwamba mja alifanya tu matendo ya sala, bali sala zitapekuliwa ili kuthibitisha usahihi wake. Kama hakufanya kwa usahihi, itakuwa kazi bure.

Sasa tujiulize, tunaposali tunatenda ndivyo? Au ndiyo tunadokoadokoa huku tukijiliwaza na kujipa matumaini kwamba Allah ni Msamehevu na Mwenye huruma hivyo atakubali sala zetu hata kama zina kasoro. Kama unafikiri hivyo basi hujafikiri sawasawa.

Katika kuonya dhidi ya kusali kwa haraka na kudokoadokoa, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: “Mwizi mbaya kuliko wote ni yule anayeiba katika sala yake.” Masahaba wakauliza: “Ewe Mtume wa Allah, anaibaje katika sala yake?” Mtume akasema: “Hakamilishi rukuu na sijida zake.”

Katika hadith nyingine iliyopokewa na Abu Huraira (Allah amridhie), imeelezwa kuwa mtu mmoja aliingia msikitini, ambamo Mtume alikuwa amekaa, akasali rakaa mbili kisha akamwendea Mtume na kumsalimia.

Mtume akajibu salamu yake kisha akamwambia: “Rudi tena ukasali kwani wewe hukusali.” Mtu yule akasali (rakaa mbili) kama alivyofanya awali, kisha akamwendea tena Mtume na kumsalimia. Mtume akajibu salamu yake na kumwambia: “Rudi tena ukasali kwani wewe hujasali.”

Mtu yule akarudi na kusali (rakaa mbili) kama alivyofanya awali, kisha akamwendea tena Mtume na kutoa salamu. Mtume akamuitikia kwa mara nyingine kisha akarejea kusema: “Rudi tena ukasali kwani wewe hukusali.”

Mtu yule akasema: “Naapa kwa Yule ambaye amekutuma wewe kwa haki. Ewe Mtume wa Allah, sijui kusali vizuri zaidi ya nilivyosali, basi nifundishe.”

Mtume akamwambia: “Ukisimama kwa ajili ya sala, sema, ‘Allahu Akbar’. Halafu soma ambacho kitakujia kwa wepesi katika Qur’an, kisha rukuu mpaka utulie katika rukuu yako. Kisha inuka na usimame wima kisawasawa, kisha sujudu mpaka utulie katika sijida yako. Kisha kaa mpaka utulie katika kikazi chako. Baada ya hapo sujudu mpaka utulie katika sijida yako, na uendelee kufanya hivyo katika sala yako yote.” [Bukhari na Muslim].

Kwa muktadha huo, yeyote atakayeendeleza tabia ya kusali sala ya ghurabu (kudokoadokoa), bila shaka atajuta Siku ya Kiyama.



Maelezo ya hadith

Hadith hii ni sahihi kabisa na imepokewa katika takriban vitabu vyote vikuu vya wanazuoni wa hadith, kikiwamo cha Bukhari, Muslim, Abu Daudi, Ibn Majah, Tirmidhi, Nasaiy na Ahmad.

Wanazuoni wengi wanaizingatia hadith hii kuwa ndiyo msingi wa

kubainisha nguzo, sunna na vitenguzi vya sala. Aidha, wanazuoni wameifanya hadith hii waliyoiita ‘Hadith ya jamaa aliyeharibu sala yake,’ kuwa rejea muhimu kila wanapoelezea sifa ya sala inayokubalika.

Tathmini ya sala zetu

Tumekwishaona madhara yanayotokana na kusali kwa kudokoadokoa. Hivyo, ni jukumu letu kufanya tathmini ya kina ya sala zetu zote, ziwe za faradhi au sunna. Tunapaswa kuazimia kutekeleza ibada ya sala ipasavyo ili tupate mafanikio na manufaa yatokanayo na ibada hii.

Vinginevyo, tutakuwa tunajiandalia maangamizi na hasara hapa duniani, kaburini na kesho Akhera. Sambamba na hilo, tunapaswa pia kujitathmini na kujiuliza kama sala zetu zinatuepusha na mambo machafu au la.

Allah anasema: “Bila shaka sala (ikisaliwa vilivyo) humzuilia (huyo mwenye kusali na) mambo machafu na maovu, na kwa hakika ndani ya sala kuna kumkumbuka Allah kuliko kukubwa kabisa...” [Qur’an, 29:45].

Isivyo bahati, wengi wetu hatuzingatii ipasavyo nguzo na sunna za sala, wala mambo yanayoweza kuiharibu. Tukirejea hadith tuliyoitaja hapo juu, tunaona jinsi Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alivyochukulia hatua makosa ya kiibada aliyoyafanya kijana aliyekwenda kumsalimia.

Hii ni dalili kuwa Mtume alikuwa makini katika kufuatilia na kuhakikisha usahihi wa ibada za wafuasi wake, jambo ambalo katika misikiti yetu limekosekana.

SAFARI YA MABADILIKO



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

ELIMU YA MAZISHI YA KIISLAMU

Chakula katika misiba: sunnah ya kuwasaidia wafiwa, sio kuwabebesha

SEHEMU YA **13**

Miongoni mwa mambo yanayoonesha uzuri wa mafundisho ya Uislamu ni namna unavyoshughulikia hali ya huzuni na udhaifu wa mwanadamu. Mtu anapofiwa na mpendwa wake, huwa katika hali ya maumivu makubwa. Wakati huo, mara nyingi hana nguvu ya kufikiria mambo mengi ya kawaida kama kupika, kuhudumia wageni au kupanga shughuli mbalimbali. Ndiyo maana Sunnah ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani) imekuja na mfumo wa huruma: jamii ndiyo imsaidie mwenye msiba, si mwenye msiba kuihudumia jamii.

Sunnah ya kuandaa chakula kwa familia ya marehemu

Baada ya kufariki Ja'far bin Abi Twalib (Allah amridhie), Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alisema: "Waandalieni familia ya Ja'far chakula, kwani wamepatwa na jambo lit-akalowashughulisha." [Abu Daud, Tirmidhiy]

Hadith hii inaweka msingi mkubwa wa kijamii: wakati wa msiba, familia ya marehemu inahitaji kusaidiwa. Kwa hiyo, majirani, ndugu na marafiki wanapowaandalia chakula wafiwa, wanafuata roho ya Sunnah.

Nani anapaswa kula chakula hicho?

Lengo la chakula hicho ni kuwasaidia wafiwa, kuwapa nguvu katika kipindi kigumu na kupunguza majukumu yao. Si lengo kuwa chakula hicho kiwe karamu au sherehe ya wageni au mkusanyiko wa kijamii.

Tatizo linapotokea

Katika baadhi ya maeneo, desturi imebadilika. Badala ya watu kusema: "Tutawaandalia chakula familia hii kwa sababu wamepata msiba," imekuwa: "Familia hii imefiwa, lazima ituandalie chakula sisi."

Hapa ndipo mzigo unapohamia upande usio sahihi. Familia iliyopoteza mpendwa wake hujikuta ikilazimika kununua chakula kingi, kuchinja wanyama, kukodisha wapishi, kukusanya fedha na wakati mwingine kukopa.

Haya yote yanafanyika wakati wao ndio wanaohitaji kusaidiwa.

Kauli ya Swahaba kuhusu kutengeneza chakula kwa wafiwa

Imepokelewa kutoka kwa Jarir bin Abdullah Al-Bajaliy (Allah amridhie): "Tulikuwa tukiona kukusanyika kwa watu kwa familia ya marehemu na kutengeneza chakula baada ya mazishi kuwa ni katika aina za maombolezo yaliyokatazwa." [Ahmad, Ibn Majah].

Wanazuoni wameeleza kwamba kilichokemewa hapa si watu kukutana kwa ajili ya kutoa pole au kusaidiana, bali ni kuifanya familia ya marehemu iwe mwenyeji wa watu na kubeba gharama za chakula wakati wa msiba.

Je, ni haramu kila chakula kinachotolewa kwa msiba?

Hapa ni muhimu kuwa na uadilifu katika kueleza. Siyo kila chakula kinachotolewa wakati wa msiba kinahukumiwa sawa.

Kuna tofauti kati ya, kwanza, chakula cha kuwasaidia wafiwa. Hiki kina msingi katika Sunnah na ni jambo jema.

Pili, familia ya marehemu kujitolea kuwalisha watu kwa nia nzuri. Hili linaweza kutokea, hasa kwa ndugu wanaokuja kutoka mbali, lakini halipaswi kuwa wajibu wala desturi inayowalazimisha watu.

Tatu, kulazimishwa kwa wafiwa kuandaa chakula kikubwa. Hili ndilo tatizo linalopaswa kurekebishwa, kwa sababu linapingana na lengo la kuwafariji wafiwa.

Suala la siku ya tatu, saba, arobaini na mwaka

Katika baadhi ya jamii zimeenea siku maalumu ambazo watu hukusanyika kwa ajili ya chakula, dua au kumbukumbu ya marehemu.

Katika suala hili, wanazuoni wametofautiana. Msingi wa tahadhari ni kwamba tusifanye siku maalumu kuwa ibada yenye fadhila maalumu isipokuwa kwa dalili.

Lakini pia marekebisho yafanywe kwa hekima, kwa sababu mara nyingi watu hufanya haya kwa sababu ya mila, huzuni au kutaka kuonesha heshima.

Njia sahihi ni kuwaelimisha watu kuhusu Sunnah ya kumuombea marehemu, kutoa sadaka kwa niaba yake kwa mujibu wa yaliyothibiti, kutekeleza madeni yake na kusaidia familia yake.

Tunapaswa kufanya nini?


Badala ya kusema: "Msifanye chakula kabisa," tunapaswa kuelekeza wale wenye uwezo wapeleke chakula kwa wafiwa, jamii ipunguze gharama za misib, familia isilazimishwe na desturi na mwisho msiba usigeuke kuwa mashindano ya kijamii.

Hitimisho

Uislamu umetufundisha kwamba huruma ya kweli ni kuubeba mzigo wa ndugu yako wakati wa udhaifu wake. Familia iliyofiwa haihitaji watu wengi wanaosubiri kuhudumiwa, bali inahitaji watu wanaosema: "Tupo pamoja nanyi. Tutawasaidia."

Huo ndio uzuri wa Sunnah ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani).

Makala ijayo: "Mambo yanayofanywa baada ya kifo: Siku ya Tatu, Saba, Mrobaini na mwaka — Mtazamo wa Sharia."



Na Aunt Samrath
0789 201 383

Waulizeni wenyewe, ikiwa yanaweza kusema!

Assalamu alaikum, watoto wangu!

Leo Aunt Samrath ana hadithi ya ajabu sana! Ni kisa cha kijana mmoja mwenye akili na ujasiri, aliyeitwa Ibrahim (amani iwe juu yake). Kijana huyu hakuogopa kuuliza maswali muhimu, hata wakati watu wengine wote waliamini jambo tofauti!

Watoto wangu, mnajua kwamba zamani kulikuwa na watu waliokuwa wakiabudu masanamu? Masanamu ni vitu vinavyotengenezwa kwa mawe, mbao au vifaa vingine na kupewa maumbo ya watu au wanyama.

Lakini hebu fikirini: Je, sanamu linaweza kuzungumza? Linaweza kusikia tunapoliita? Linaweza kutusaidia?

Hebu tusikilize!

Ibrahim auliza maswali ya akili

Zamani, Nabii Ibrahim aliishi miongoni mwa watu waliokuwa wakiabudu masanamu waliyoyatengeneza kwa mikono yao wenyewe.

Lakini Ibrahim alijua kwamba vitu vinavyotengenezwa na binadamu haviwezi kuwa miungu. Allah pekee ndiye anayestahili kuabudiwa.

Siku moja, akawauliza watu wake:

“Haya ni masanamu gani mnayoyaabudu?”

Wakamjibu:

“Tuliwakuta baba zetu wakiyaabudu.”

Ibrahim akawaambia waziwazi: “Hakika nyinyi na baba zenu mmekuwa katika upotovu ulio wazi!”

Lakini watu wake hawakutaka kuachana na masanamu yao.

Mpango wa ajabu!

Siku moja, watu walipoondoka, Ibrahim akaenda mahali yalipokuwa masanamu yao.

Akayavunja yote, isipokuwa lile kubwa kuliko mengine!

Watu waliporudi, wakashangaa sana!

“Nani ameyafanya haya masanamu yetu?” wakaulizana kwa hasira.

Baadhi yao wakasema: “Tulimsikia kijana mmoja anayeitwa Ibrahim akiyazungumzia!”

Basi, wakamleta Ibrahim mbele yao na kumuuliza:m“Ewe Ibrahim! Je, wewe ndiye uliyefanya hivi kwa miungu yetu?”

Ibrahim akawajibu: “Bali limefanya hili kubwa lao! Basi yaulizeni, ikiwa yanaweza kusema!”

Lo! Watoto wangu, mnadhani masanamu yalijibu?

Hapana! Hata moja halikusema kitu!

Ukweli unajulikana!

Watoto wangu, mnajua kilichotokea?

Watu wale wakaanza kutafakari. Wakajua kwamba walikuwa wamekosea!

Lakini badala ya kukubali ukweli, wakamwambia Ibrahim: “Unajua kabisa kwamba haya hayasemi!”

Hapo ndipo Ibrahim alipowauliza swali muhimu zaidi: “Basi, kwa nini mnaabudu badala ya Allah vitu ambavyo haviwezi kuwanufaisha wala kuwadhuru?”

Watoto wangu, hilo lilikuwa swali la kufikirisha sana!

Ikiwa masanamu hayawezi kuzungumza, kujisaidia wala kuwalinda watu, kwa nini yaabudiwe?

Allah amnusuru Ibrahim!

Lakini watu wale hawakukubali. Badala yake, wakakasirika na kuamua kumwadhibu Ibrahim kwa kumtupa motoni!

Wakawasha moto mkubwa!

Watoto wangu, mnajua moto unaweza kuunguza, sivyo?

Lakini Allah ana uwezo juu ya kila kitu!

Allah akauamrisha moto: “Ewe moto! Kuwa baridi na salama kwa Ibrahim!”

Subhanallah!

Kwa amri ya Allah, moto haukumdhuru Ibrahim!

Watu walitaka kumdhuru, lakini Allah akamnusuru.

Tunajifunza nini?

Watoto wangu, kisa hiki kinatufundisha mambo matatu muhimu sana!

Kwanza, Allah pekee ndiye anayestahili kuabudiwa. Yeye ndiye Muumba wa jua, mwezi, nyota, miti, wanyama na kila kitu! Masanamu hayawezi kuumba chochote.

Pili, tusifuate mambo bila kufikiri. Kama Ibrahim, tujifunze kuuliza maswali na kutafuta ukweli. Rafiki yako akifanya jambo baya, usimfuate kwa sababu tu wengine wanafanya hivyo.

Tatu, tumtegemee Allah. Tunapokutana na matatizo au kuogopa jambo fulani, tumuombe Allah atusaidie. Pia tuwaambie wazazi wetu au watu wazima tunaowaamini tunapokuwa hatarini.

Kumbukeni, watoto wangu, kusema ukweli kunahitaji ujasiri. Lakini tunapaswa kusema ukweli kwa hekima na heshima.

٧ جمادى الآخرة ١٤٤٨هـ

UCHAMBUZI

Na Said Rajab
0783 650 803

Siasa za Magharibi na hatima ya uhuru wa Dini

Marufuku ya uvaaji wa hijab shuleni imezua taharuki nchini Azerbaijan wiki iliyopita, ambapo maelfu ya wananchi waliandamana kupinga sheria inayowazuia wanafunzi na walimu kuvaa vazi hilo katika taasisi za elimu.

Video zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii ziliwaonesha wanafunzi wakiwakumbatia walimu wao huku wakibubujikwa na machozi wakati walimu hao wakiondolewa katika maeneo ya shule.

Hatua hiyo imeibua mjadala mpana kuhusu uhuru wa dini, haki ya kupata elimu na nafasi ya imani katika mifumo ya utawala wa kisekula. Katika kupinga hatua hiyo, wanafunzi wengi walisusia masomo wakitaka wenzao waliovaa hijab waruhusiwe kurejea shuleni na kuendelea na masomo yao.

Mnamo Oktoba 12 mwaka huu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Azerbaijan, nchi yenye wakazi wengi Waislamu, ilisema kuwa watu 37 waliokuwa wakishiriki katika maandamano hayo walikamatwa katika mji mkuu wa Baku pekee. Hata hivyo, wanaharakati waliripoti kuwa zaidi ya watu 200 walikamatwa kote nchini.

Miongoni mwa waliokamatwa ni Shahizyar Huseynova, mama aliyekamatwa baada ya kushiriki maandamano yaliyofanyika nje ya shule moja jijini Baku, kufuatia binti yake kuzuiwa kuingia darasani. Kwa mujibu wa mumewe, Huseynova amekuwa kizuizini kwa muda wa miezi minne bila kufunguliwa mashtaka yoyote dhidi yake.

Huseynova ni mwanaharakati aliyeanzisha jukwaa la bure la mtandaoni linalowaunganisha walimu wa kujitolea na watoto waliotengwa na mfumo wa elimu, wakiwamo wale waliofukuzwa shuleni kwa sababu ya kuvaa hijab.

Alitoweka Oktoba 14 mwaka huu, huku taarifa zikidai kuwa alikamatwa na mamlaka za Azerbaijan. Mwezi Septemba mwaka huu, Baraza la Mawaziri la Azerbaijan lilipitisha Azimio Namba 309, lililofanyia marekebisho mwongozo wa sare za wanafunzi katika taasisi za elimu za umma.

Marekebisho hayo yanapiga marufuku mavazi ya shule yanayokwenda kinyume na misingi ya kisekula inayozingatiwa na Serikali ya nchi hiyo. Oktoba 9 mwaka huu, Idara ya Elimu ya jiji la Baku ilitangaza rasmi kuanza kufuatilia utekelezaji wa kanuni hiyo ya mavazi ya kisekula katika shule zote za umma.

Ndugu zangu, marufuku ya kuvaa hijab shuleni nchini Azerbaijan inaibua hoja kuhusu uhusiano kati ya utawala wa kisekula na Uislamu.

Ni wazi kwamba itikadi na mfumo wa kisekula haviendani na misingi ya Uislamu. Kimsingi, usekula unakinzana na baadhi ya kanuni na sheria za Uislamu.

Hivyo, ni dhahiri kuwa mfumo huo haufai kutumika katika kuongoza nchi zenye Waislamu wengi. Ni mfumo unaowafukuza wasichana na wanawake shuleni na kazini kwa sababu tu ya kutii amri ya Mola wao kuhusu mavazi, huku ukiwafunga Waislamu wengine kwa sababu ya jitihada zao za kulinda dini yao.

Ni mfumo unaoruhusu aina mbalimbali za maovu katika jamii, yakiwamo matumizi ya pombe na uhusiano haramu, huku ukipiga marufuku mambo yanayohusishwa na haki na heshima, kama vile kuvaa hijab.

Ni mfumo unaodai kuwa, wanadamu, licha ya kuwa na uwezo mdogo wa kufikiri na kubadili misimamo yao mara kwa mara, wana mamlaka makubwa zaidi ya kutunga sheria zinazosimamia maisha ya watu kuliko Muumba wao, ambaye ni Mjuzi wa yote na Mwenye hekima isiyo na kifani.

Ni mfumo unaodai kuwa dini haipaswi kupewa nafasi katika shule, sehemu za kazi au taasisi za umma. Msimamo huo unakinzana na mafundisho ya Mwenyezi Mungu, ambaye ameiteremsha dini yenye sharia na mwongozo unaosimamia kila nyanja ya maisha ya mwanadamu, ikiwamo siasa, uchumi, masuala ya kijamii na elimu.

Kwa mtazamo huo, dini na dola haviwezi kutenganishwa, kama inavyosisitizwa katika Qur'an: "Na tumekuteremshia Kitabu hiki kinachobainisha kila kitu, na ni uongofu, rehema na bishara kwa Waislamu." [Qur'an, 16:89].

Mfumo wa kisekula umeshindwa kuhakikisha hata haki za msingi za wanawake na wasichana wa Kiislamu. Badala yake, unawawekea vikwazo vinavyowanyima fursa za kupata elimu, ajira na hata uhuru wa kutembea kwa sababu tu ya kuvaa mavazi yao ya Kiislamu.



٧ جمادى الآخرة ١٤٤٨هـ

UCHAMBUZI

Na Said Rajab
0783 650 803



Dunia inahitaji mfumo wa kiuchumi wa Kiislamu

SEHEMU YA 1

Miongoni mwa neema kubwa alizowajalia Mwenyezi Mungu wanadamu ni kumtuma Mtume Muhammad (rehema na amani za Allah zimshukie) akiwa na ujumbe wa Uislamu, uliojengwa juu ya misingi ya mwongozo, rehema na nuru.

Ujumbe huo umekuwa rehema kwa masikini na matajiri, huku ukihakikisha haki inatendeka kwa wanyonge na wenye nguvu bila ubaguzi. Hili linathibitishwa na kauli ya Allah Ta'ala isemayo: "Hiki ni Kitabu tulichokiteremsha kwako (Muhammad) ili uwatoe watu gizani na kuwaingiza katika nuru, kwa idhini ya Mola wao, na uwaongoze kwenye njia ya Mwenye nguvu, Msifiwa." [Qur'an, 14:1].

Wanadamu wamenufaika na mwongozo huo kwa takriban karne 13, katika kipindi ambacho Uislamu umekuwa msingi wa mfumo wa utawala na uendeshaji wa dola. Hali hiyo iliendelea hadi mwanzoni mwa karne iliyopita, wakati dola ya Kiislamu ilipobomolewa na Uislamu kuondolewa katika mfumo wa utawala.

Ukomunisti na ubepari vilitawala dunia katika vipindi tofauti. Hata hivyo, baada ya kudhoofika kwa mfumo wa kikomunisti, ubepari umebaki kuwa mfumo mkuu wa kiuchumi unaotawala sehemu kubwa ya dunia, huku mamilioni ya watu wakiendelea kukabiliwa na maisha magumu.

Hivi karibuni, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) lilitangaza takwimu zinazoonesha kuwa idadi ya watu wanaoishi katika umasikini duniani imefikia bilioni 1.2, kwa mujibu wa Kipimo cha Umasikini Duniani (Global Poverty Index).

Idadi hiyo ni zaidi ya moja ya nane ya watu wote duniani, ambao wanakadiriwa kufikia bilioni nane. Hali hii inajitokeza licha ya ukweli kwamba mstari rasmi wa umasikini wa kimataifa, uliowekwa na Benki ya Dunia na Umoja wa Mataifa ni dola tatu tu kwa mtu kwa siku.

Katika toleo la mwaka 2026 la ripoti yao ya kila mwaka, UNDP kwa kushirikiana na Kituo cha Utafiti cha Oxford Poverty and Human Development Initiative (OPHI), wamerekodi ongezeko la watu milioni 51.5 wanaokabiliwa na umasikini uliokithiri ikilinganishwa na mwaka uliotangulia.

Kwa mujibu wa mashirika hayo mawili, ongezeko hilo ni la kwanza kurekodiwa katika kipindi cha miaka 16. Hali hii inajitokeza licha ya kuongezeka kwa uzalishaji na kupanuka kwa uchumi wa dunia, maendeleo ambayo hayajawanufaisha watu wengi, hususan masikini na wale wanaoishi katika mazingira magumu.

Licha ya maendeleo makubwa ya kiteknolojia na ukuaji wa kasi wa uchumi, mafanikio hayo bado hayajawanufaisha watu hao kwa kiwango kinachokidhi mahitaji yao ya msingi. Hadi sasa, maendeleo hayo hayajaweza kuhakikisha upatikanaji wa mahitaji muhimu ya maisha, yakiwamo chakula, mavazi, makazi, elimu, huduma za afya na usalama.


Msimamizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP), Alexander De Croo, alisema katika taarifa yake kuwa ongezeko la umasikini linapaswa kuwa wito wa kuamsha dunia na kuchochea hatua za kukabiliana na hali hiyo.

Aliongeza kuwa takwimu za UNDP na OPHI zinaonesha hali halisi ya maisha ya watu bilioni 1.2 wanaokabiliwa na changamoto mbalimbali zinazohusiana, zikiwamo njaa, ukosefu wa fursa za elimu, maji safi na huduma za umeme.

Itaendelea wiki ijayo Insha Allah

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

٧ جمادى الآخرة ١٤٤٨هـ



MAISHA YA MTUME AYUB NA KAUMU YAKE

SEHEMU YA 2

Kama tulivyoashiria katika toleo lililopita, Allah Mtukufu alimneemesha Nabii Ayub (amani ya Allah iwe juu yake) kwa mali nyingi za aina mbalimbali na yeye alikuwa akitumia mali hizo kuwasaidia mafukara, masikini, wajane, mayatima, jamaa zake, wageni, wasafiri na watu waliokuwa katika hali ngumu ya maisha.
Lakini Allah, kwa hekima yake, akataka kumjaribu mja wake huyo kama alivyowajaribu waja wake wengine wema, ili kudhihirisha subira yake wakati wa shida, kama ilivyodhihirika shukrani yake wakati wa raha na neema.

Basi, Nabii Ayub akajaribiwa kwa kuondokewa na mali zake, watoto na watu wake, kisha akapatwa na maradhi makubwa katika mwili wake.

Katika baadhi ya simulizi za wanazuoni wa tafsiri, inaelezwa kuwa mwili wake ulijaa vidonda na maradhi yakazidi kuwa makali. Hali yake ikawa ngumu kiasi kwamba watu wake wa karibu na marafiki wakajitenga naye. Jamaa zake wakamtoa nje ya mji, akabaki na mkewe pekee aliyeendelea kumhudumia.

Maradhi hayo hayakudumu kwa siku moja, mwezi mmoja au mwaka mmoja, bali kwa miaka kadhaa.

Anas bin Malik (Allah awe radhi naye) amesimulia kutoka kwa Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amanu) kwamba amesema: “Hakika Ayub, Nabii wa Allah, alikaa katika mtihani wake miaka 18, mpaka akatengwa na watu wa karibu na wa mbali.” [Ibn Hibban].

Imam Ibn Kathir, katika tafsiri yake, ameeleza kuwa Nabii Ayub alijaribiwa kwa kuondokewa na mali, watoto na afya yake. Alikuwa na mifugo, mashamba, watoto na majumba mazuri, lakini neema hizo zikamuondokea.

Aidha, alinukuu simulizi kwamba maradhi yalimwathiri mwili wake, huku moyo na ulimi wake vikiendelea kumtaja Allah. Watu wake walijitenga naye, lakini mkewe aliendelea kumtunza na kumhudumia. [Tafsir Ibn Kathir].

Pamoja na mitihani hiyo, Nabii Ayub aliendelea kuwa na subira, kumtaja Allah na kutarajia rehema na faraja kutoka kwa Mola wake.

Nabii Ayub afundishwa namna ya kuomba

Baada ya kipindi kirefu cha majaribu, Nabii Ayub alimuelekea Allah Mtukufu kwa dua iliyoonyesha unyenyekevu mkubwa mbele ya Mola wake. Dua hiyo ilidhihirisha ufahamu wake kwamba hakuna mwenye uwezo wa kuondoa madhara na kuleta faraja isipokuwa Allah.

Yeye, Allah, ndiye Mwenye uwezo wa kutoa na kuzuia, kuleta na kuondoa, kusikia maombi ya waja wake na kutekeleza analolitaka. Imani na yakini hiyo ndiyo iliyokuwa imetawala moyo wa Nabii Ayub na kumjengea matumaini ya kupata faraja kutoka kwa Mola wake.

Allah Mtukufu anasema: “Na (mtaje) Ayub alipomwita Mola wake (akasema): ‘Hakika imenipata dhara, nawe ndiye Mwenye kurehemu kuliko wote wanaorehemu.’” [Qur’an, 21:83]. Katika maombi haya, Nabii Ayub alionyesha adabu kubwa mbele ya Mola wake. Alieleza hali ya dhiki na mateso yaliyomfika, lakini hakutaja moja kwa moja ombi la kuponywa.

Hii inaonyesha kiwango cha subira yake, dhana njema aliyokuwa nayo kwa Allah na kutoridhika kwake na dhara hakukumfanya akate tamaa na rehema za Mola wake.

Nabii Ayub afikiwa na faraja

Baada ya subira hiyo kubwa, Allah Mtukufu alimkubalia dua yake na kumuondolea madhara yaliyokuwa yamemfika.

Allah anasema: “Basi tukamkubalia na tukamuondolea dhara aliyokuwa nayo, na tukampa watu wake na mfano wao pamoja nao, kwa rehema itokayo kwetu na ili iwe ukumbusho kwa wafanyao ibada.” [Qur’an, 21:84].

VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

Katika aya nyingine, Allah anasema: “Na mkumbuke mja wetu Ayub alipomwita Mola wake (akasema): ‘Hakika Shetani amenifikishia udhia na mateso.’” [Qur’an, 38:41].

Aya hizi zinaonyesha namna Allah alivyomrehemu mja wake baada ya kuvumilia mitihani iliyomfika.

Nabii Ayub apatiwa tiba

Allah Mtukufu hakumkubalia tu dua ya Nabii Ayub, bali alimuelekeza pia namna ya kujitibu. Alimwamrisha apige ardhi kwa mguu wake, na hapo yakapatikana maji yaliyokuwa tiba ya maradhi yake. Allah anasema: “Piga chini kwa mguu wako. Haya ni maji baridi ya kuogea na kunywa.” [Qur’an, 38:42].

Nabii Ayub alifuata maelekezo hayo ya Mola wake. Akaoga na kunywa maji yale, na kwa uwezo wa Allah, maradhi yakamuondokea na afya yake ikarejea kama ilivyokuwa kabla.

Allahu Akbar!

Si afya yake pekee iliyorejeshwa. Allah alimrejeshea pia watu wake na kumpa wengine mfano wao, kama ilivyoelezwa katika Qur’an.

Sheikh Abdurahman Nasir As-Sa’di (Allah amrehemu) amesema kwamba Allah alimrejeshea Nabii Ayub watu wake, akampa wengine mfano wao na akamruzuku utajiri mkubwa. [Taysir Al-Karim Ar-Rahman, uk. 681].

Nabii Ayub na kiapo kuhusu mkewe

Katika simulizi ya Nabii Ayub, kuna pia tukio linalohusu kiapo alichokuwa amekiapa kuhusu mkewe. Sheikh As-Sa’di, akinukuu maelezo ya wanazuoni wa tafsiri, amesema kuwa Nabii Ayub alipokuwa mgonjwa, siku moja alimkasirikia mkewe kutokana na jambo fulani na kuapa kwamba Allah akimponyesha, angempa viboko mia moja.

٧ جمادى الآخرة ١٤٤٨هـ

TAFAKURI YA WIKI

NA SAMRATH MSUYA
0789 201 383

Nini kifanyike kukuza uelewa wa huduma za fedha za Kiislamu?



Ukisikiliza karibu kila wasilisho kuhusu maendeleo ya huduma za fedha za Kiislamu nchini Tanzania, kuna changamoto moja inayojirudia: uelewa mdogo wa wananchi kuhusu huduma hizo.

Ilikuwa hivyo pia katika Kongamano la Uwekezaji Halal lililofanyika wiki hii. Salum Awadh aliitaja changamoto hiyo katika wasilisho lake kuhusu “Hali ya Sekta ya Fedha za Kiislamu Afrika Mashariki,” kama alivyofanya Sheikh Mohamed Issa katika mada yake kuhusu “Fedha za Kiislamu: Mwenendo wa Kimataifa na Mafunzo kwa Tanzania.”

Iwe ni benki za Kiislamu, bima ya Takaful au uwekezaji unaozingatia Sharia, tatizo ni lilelile. Wananchi wengi hawafahamu vizuri huduma hizi, namna zinavyofanya kazi na manufaa yake.

Kinachonishangaza ni kwamba tatizo hili limekuwa likitajwa kwa miaka mingi. Hata suluhisho lake linajulikana: kuongeza elimu kwa wananchi.

Swali langu ni hili: Ikiwa tunalijua tatizo na suluhisho lake, kwa nini bado tunalirudia katika kila mkutano? Huenda kinachokosekana ni mikakati madhubuti, endelevu na inayoratibiwa vizuri.

Tatizo si kutokujua pekee

Wapo wananchi wasiofahamu kabisa uwepo wa huduma hizi. Lakini hata miongoni mwa wanaozifahamu, baadhi wana uelewa usio sahihi.

Kwa mfano, wengine wanaamini huduma za fedha za Kiislamu ni za Waislamu pekee. Wengine hudhani benki za Kiislamu zina riba ileile ya benki za kawaida, isipokuwa imepewa majina ya Kiarabu.

Dhana hizi zinahitaji kujibiwa kwa elimu. Wananchi wanahitaji kuelewa tofauti kati ya riba na faida ya biashara halali, namna mikataba inavyofanya kazi na misingi ya kuthibitisha uhalali wake.

Ni wangapi wanaofahamu Takaful na tofauti yake na bima ya kawaida? Vipi kuhusu Waqf na nafasi yake katika maendeleo ya jamii? Au Zaka kama wajibu wa kidini wenye masharti na makundi maalumu ya wanufaika?

Hata elimu ya uwekezaji inahitaji kuimarishwa. Leo, wataalamu wa fedha mitandaoni wanahamasisha wananchi kuwekeza katika mifuko ya pamoja ya uwekezaji. Hilo ni jambo jema.

Lakini je kuna nguvu inayolingana na ushawishi wa walimu hao ya kuwafahamisha wananchi kama mifuko hiyo inaendana na Sharia? Kwa Mwislamu, kujua faida inayotarajiwa hakutoshi. Anahitaji pia kuelewa fedha zake zinawekezwa wapi na kwa mikataba gani.

Si sahihi kusema kila mfuko huo ni halali au haramu bila kuchunguza shughuli na muundo wake.

Elimu inawafikia akina nani?

Ni kweli, juhudi za kutoa elimu zinafanyika. Kuna semina, makongamano, mihadhara na vipindi vya vyombo vya habari. Lakini tunapaswa kujiuliza: Je, tunawafikia watu wapya au tunaendelea kuwaelimisha watu wa kada zilezile?

Huenda washiriki wa makongamano mengi ni wataalamu, viongozi wa taasisi na watu ambao tayari wana ufahamu fulani kuhusu fedha za Kiislamu. Wakati huohuo, makundi makubwa ya wananchi yanaweza kuwa hayajafikiwa.

Kuyafikia kunahitaji zaidi ya kuandaa semina. Kunahitaji utaalamu wa mawasiliano: kutambua makundi ambayo hayajafikiwa, kuelewa mahitaji yao ya taarifa na kufahamu majukwaa ya vyombo vya habari wanayoyatumia.

Elimu yenye mafanikio si ile inayotolewa mara nyingi, bali inayowafikia watu wanaoihitaji na kubadilisha uelewa wao.

Kuuza bidhaa au kujenga uelewa?

Taasisi za fedha zina sababu za kutangaza bidhaa zao. Zinahitaji wateja na ukuaji wa biashara. Lakini matangazo ya bidhaa hayawezi kuchukua nafasi ya elimu pana.

Kampeni ya elimu kuhusu mfumo mzima inawanufaisha wananchi na watoa huduma wote. Mtu anayeelewa thamani ya bidhaa hahitaji nguvu nyingi kushawishiwa kuitumia.

Zaidi ya biashara, hapa kuna wajibu wa kidini wa kuwaelimisha watu kuhusu njia halali za kupata, kutumia na kuendeleza mali. Masheikh na wanazuoni washirikiane na wataalamu wa fedha ili elimu iwe sahihi kidini na kitaalamu.

CIFCA iongoze juhudi hizi

Ninaamini Kituo cha Ushauri na Uzingatiaji wa Sheria za Fedha za Kiislamu (CIFCA) kina nafasi muhimu ya kuhamasisha na kuratibu kampeni ya pamoja ya elimu kwa umma.

Kinachohitajika ni mkakati wa muda mrefu, wenye walengwa, njia za kuwafikia na malengo yanayopimika.

Fedha zinaweza kutafutwa kwa ushirikiano na benki, taasisi za Takaful, kampuni za uwekezaji na wadau wengine. Misikiti, madrasa, vyuo, redio, televisheni na mitandao ya kijamii vitumike kuwafikia wananchi wa kada na imani mbalimbali.

٧ جمادى الآخرة ١٤٤٨هـ

NA ZAHARANI BARAKA

MATUKIO YENYE MAZINGATIO

Makosa katika fat–wa na athari zake kwa jamii

Mtu mmoja alimwendea mwanazuoni mashuhuri, Al–Izz Ibn Abdus–Salaam, anayejulikana kwa jina la Sultani wa Wanazuoni na kumuuliza kuhusu jambo fulani. Al–Izz (Allah amrehemu) alimjibu kwa kutoa fat–wa, lakini mtu huyo alipoondoka aligundua kuwa fat–wa aliyokuwa ametoa ilikuwa na makosa.

Hata hivyo, hakung'ang'ania msimamo wake, bali alikiri kosa hilo bila kusita. Baadaye alimlipa mtu ili azunguke katika maeneo mbalimbali ya nchi na kutangaza: "Yeyote aliyemuuliza (Al–Izz) kuhusu jambo lolote, asifanyie kazi fat–wa aliyompa kwa kuwa ina makosa."

Kwa kufanya hivyo, Al–Izz alionesha kuwa heshima, cheo, elimu wala aibu ya kukiri kosa havipaswi kumzuia mtu kurejea kwenye ukweli. [Taz: 'Mausu'at al–akhlaq wazzuhd warraqaiq']

Mafundisho ya tukio

Katika zama hizi za teknolojia na mitandao ya kijamii, kila mtu ana nafasi ya kutoa maoni kuhusu masuala mbalimbali. Hata hivyo, hali inatia wasiwasi zaidi pale watu wanapozungumzia dini ya Allah bila kuwa na elimu sahihi.

Baadhi yao huthubutu kutoa fat–wa, kuhalalisha au kuharamisha mambo bila kurejea dalili na misingi ya kielimu. Historia ya Uislamu inatufundisha kuwa wanazuoni wema walikuwa na tahadhari kubwa wali-pozungumzia masuala ya dini.

Walipobaini kuwa wamekosea, hawakusita kukiri na kurekebisha makosa yao. Kutokana na mwenendo huo, tunapata mafunzo muhimu yafuatayo:

Mosi, kukiri kosa ni sehemu ya ujasiri

Kukiri kosa si udhaifu bali ni ishara ya ujasiri, ukomavu na uaminifu katika dini. Ujasiri haupimwi kwa uwezo wa kukabiliana na wengine pekee, bali pia kwa uwezo wa kuishinda nafsi, kukubali makosa na kusimamia ukweli.

Ikiwa wanazuoni wakubwa hawakusita kukiri makosa yao, kwa nini baadhi ya watu leo hutumia dini kujitafutia umaarufu kwa kutoa fat–wa zisizo na msingi na kusambaza taarifa zisizo sahihi.

Pili, ukweli ni muhimu kuliko heshima ya mtu

Al–Izz alikuwa mwanazuoni mashuhuri, lakini hakuruhusu cheo chake kimzuie kukiri kosa. Hii inatufundisha kuwa dalili na ukweli vinapaswa kutangulizwa kuliko misimamo ya watu. Kunyamazia kosa baada ya kulibaini ni kukiuka wajibu wa kusimamia haki.

Tatu, mwanazuoni anapaswa kurekebisha makosa yake

Makosa katika fat–wa yanaweza kuwaathiri watu wengi. Hivyo, mwanazuoni anapobaini kuwa amekosea anapaswa kurekebisha hukumu hiyo. Huu ni mwenendo unaopaswa kuigwa na wanazuoni, walimu na walinganiaji.

Nne, aibu isiwe kikwazo cha kurejea kwenye haki

Baadhi ya watu wenye vyeo na heshima katika jamii husita kukiri makosa kwa kuhofia kupoteza hadhi zao. Kimsingi, aibu haipaswi kuwa kisingizio cha kuukataa ukweli.

Muislamu anapaswa kuwa tayari kuacha msimamo wake pale ukweli unapomdhihirikia. Allah anasema: "Wala msichanganye haki na batili, wala msifiche ukweli hali ya kuwa mnaujua." [Qur'an, 2:42].

Aidha, Mtume (rehema na amani za Allah zimshukie) amesema: "Hakuna husuda inayofaa isipokuwa katika mambo mawili: Mtu ambaye Allah amempa mali, naye akaitumia katika haki; na mtu ambaye Allah amempa elimu, naye anahukumu kwa kutumia elimu hiyo na kuwafundisha wengine." [Bukhari na Muslim].

Imam Malik pia aliwahi kusema: "Kila mtu kauli yake inaweza kukubaliwa au kukataliwa, isipokuwa mwenye kaburi hili," akimaanisha Mtume Muhammad (rehema na amani zimshukie). Hii inathibitisha kuwa kipimo cha mwisho cha haki ni Qur'an na Sunna sahihi, si misimamo ya watu.

Ujumbe huu ni muhimu kwa walimu, maimamu, wanazuoni na walinganiaji. Mwalimu anapokosea akubali kurekebishwa; Imam anapobaini kosa katika hukumu yake arejee kwenye usahihi; na mwenye kutoa fat–wa anapogundua kuwa amekosea asisite kutangaza marekebisho.

Kuna tofauti kati ya mtu anayependa kuonekana kuwa sahihi na yule anayethamini ukweli. Wa kwanza hung'ang'ania kauli yake hata pale anapobaini kuwa amekosea, kwa sababu kwake kukiri kosa ni sawa na kukubali kushindwa.

Wa pili huwa tayari kubadili msimamo wake mara tu ukweli unapodhihirika, kwa sababu ukweli una thamani kubwa kwake kuliko kushikilia msimamo usio sahihi.

Allah anasema: "Sema: Hakika Mola wangu ameharamisha mambo machafu, yaliyo wazi na yaliyofichikana, na dhambi, na uadui bila haki, na kumshirikisha Allah na kile ambacho hakukiteremshia dalili yoyote, na kusema juu ya Allah yale msiyoyajua." [Qur'an, 7:33].

Katika aya nyingine Allah anasema: "Na miongoni mwa watu wapo wanaowapoteza wengine kutoka katika njia ya Allah bila elimu, na wanaifanya njia hiyo kuwa ni mzaha. Hao watapata adhabu yenye kudhalilisha." [Qur'an, 31:6].

Kwa hiyo, Muislamu anapaswa kuwa na tahadhari kabla ya kutoa hukumu kuhusu halali na haramu. Mtu anayejadili masuala ya dini bila elimu ya kutosha anaweza kuwapotosha wengine na hata kujipotosha mwenyewe, huku akichangia watu kuiacha haki na kupotea katika njia iliyo sahihi.

UONGOZI UTAWALA

Na Ukhti Fatima SS

0789 201 383

Kwa nini wafanyakazi wazuri huondoka kwenye taasisi yako?

Una mfanyakazi mwenye uwezo mkubwa, mwadilifu na anayejituma. Anatimiza majukumu yake vizuri, anaheshimu muda na mara nyingi hufanya hata zaidi ya anachotarajiwa. Siku moja anakuletea barua ya kuacha kazi. Unashangaa. Unajiuliza kwa nini anaondoka wakati taasisi inamhitaji sana. Hali hii hutokea katika kampuni, taasisi za serikali, mashirika na hata taasisi zisizo za faida. Viongozi huwekeza muda na fedha kuajiri na kuwafundisha wafanyakazi, lakini wakati mwingine hushindwa kuwafanya waendelee kufanya kazi katika taasisi zao.

Sababu za kuondoka kazini hutofautiana. Wengine hutafuta mishahara mikubwa, wengine nafasi bora za maendeleo, huku baadhi wakiondoka kwa sababu ya mazingira yasiyoridhisha ya kazi.

Lakini kuna jambo ambalo viongozi wanapaswa kuelewa: Wafanyakazi wazuri hawabaki kazini kwa sababu ya mshahara pekee. Wanahitaji pia kuheshimiwa, kuthaminiwa, kuaminiwa na kuona mustakabali wao katika taasisi.

Mshahara ni muhimu, lakini hautoshi

Hakuna sababu ya kupuuza umuhimu wa mshahara mzuri.

Mfanyakazi ana mahitaji ya familia, gharama za maisha na malengo ya kifedha. Anapohisi kuwa malipo yake hayalingani na majukumu au thamani ya kazi yake, anaweza kuanza kutafuta fursa nyingine.

Hata hivyo, mshahara mkubwa hauwezi kufidia kila tatizo la mahali pa kazi.

Mfanyakazi anayelipwa vizuri lakini hudhalilishwa, hapewi nafasi ya kutoa maoni au anaishi kwa hofu ya mkuu wake anaweza kuamua kuondoka.

Ndiyo maana taasisi zinapaswa kuangalia malipo pamoja na mazingira ya kazi, usalama wa ajira, haki na fursa za maendeleo.

Watu wanataka kuthaminiwa, si kutumiwa tu

Fikiria mfanyakazi ambaye amefanya kazi kwa bidii kukamilisha mradi muhimu. Ameongeza muda wa kazi, ameshirikiana na wenzake na hatimaye mradi umefanikiwa.

Lakini hakuna anayemtambua. Hakuna pongezi, shukrani wala mazungumzo kuhusu mchango wake. Baada ya muda, anaweza kuanza kujiuliza kama juhudi zake zina maana.

Kutambua mchango wa mfanyakazi si lazima kuhusishe zawadi kubwa au fedha.

Wakati mwingine kumshukuru hadharani, kutambua mafanikio yake au kumweleza namna kazi yake ilivyosaidia taasisi kunaweza kumtia moyo.

Hata hivyo, pongezi hazipaswi kutumiwa kama mbadala wa malipo ya haki.

Kusikilizwa kunajenga uaminifu

Katika baadhi ya taasisi, viongozi huzungumza na wafanyakazi pale tu wanapotaka kutoa maagizo.

Mfanyakazi anapokuwa na pendekezo, malalamiko au changamoto, anakosa nafasi ya kueleza.

Hali hii inaweza kumfanya ajisikie kuwa maoni yake hayana thamani.

Kiongozi anayewasikiliza wafanyakazi anaweza kugundua matatizo ambayo hayafiki katika ripoti rasmi.

Lakini kusikiliza hakumaanishi kukubaliana na kila pendekezo.

Muhimu ni kutoa nafasi ya mazungumzo ya kweli, kueleza sababu za maamuzi na kuchukua hatua pale inapowezekana.

Kuamini wafanyakazi kunawapa nguvu

Wapo viongozi wanaotaka kufuatilia kila hatua ya wafanyakazi wao.

Wanatoa jukumu, lakini hawaruhusu mfanyakazi aamue namna ya kulitekeleza. Kila jambo dogo lazima lipate idhini yao.

Mtindo huu unaweza kuwafanya wafanyakazi wajisikie hawana uwezo au hawaaminiki.

Mfanyakazi mwenye ujuzi anahitaji nafasi ya kutumia maarifa yake, kufanya maamuzi yanayoendana na wajibu wake na kuwajibika kwa matokeo.

Kiongozi anaweza kuweka malengo na viwango vya kazi bila kudhibiti kila hatua.

Kumpa mfanyakazi uhuru unaoendana na uwezo wake ni namna ya kuonyesha uaminifu na kumjengea kujiamini.


Wafanyakazi wanataka kuona wanakokwenda

Mfanyakazi anaweza kuipenda kazi yake, lakini akachoka kufanya majukumu yaleyale kwa miaka mingi bila kujifunza jambo jipya.

Watu wengi hutamani kuongeza ujuzi, kukabiliana na changamoto mpya na kupata nafasi za maendeleo.

Taasisi inayowekeza katika mafunzo, ushauri wa kitaaluma na kukuza uwezo wa wafanyakazi inaongeza sababu zinazoweza kuwafanya waendelee kubaki.

Kiongozi anaweza kuanza kwa kumuuliza mfanyakazi anataka kuwa wapi kitaaluma katika miaka michache ijayo.



MAKALA MALEZI

NA JUNAYNAT ALLY DAMA

0789 201 383

Mambo 10 madogo yatakayoacha athari chanya kwa mtoto wako!

Wazazi wengi wanatamani kuwapa watoto wao maisha mazuri. Wanahangaika kutafuta fedha za chakula, mavazi, elimu bora na mahitaji mengine. Wengine huwanunulia midoli ya gharama kubwa, simu na zawadi mbalimbali ili kuwafurahisha.

Lakini je, umewahi kufikiria kwamba baadhi ya mambo ambayo mtoto wako atayakumbuka kwa muda mrefu huenda hayakukugharimu hata shilingi moja?

Kumbatio la asubuhi, maneno ya upendo, dakika chache za kucheza pamoja au kumpongeza kwa jambo dogo vinaweza kuwa na maana kubwa kuliko tunavyodhani.

Katika makala iliyochapishwa kwenye tovuti ya Parent From Heart, Julai 20, 2024, mwandishi Mikko Pornel anaeleza namna vitendo vidogo vya kila siku vinavyoweza kuimarisha uhusiano kati ya wazazi na watoto.

Maneno machache yenye maana kubwa

Ni lini mara ya mwisho ulimwambia mtoto wako unampenda?

Baadhi ya wazazi huamini kwamba mtoto anajua anapendwa kwa sababu anapatiwa chakula, mavazi na elimu. Lakini watoto wanahitaji pia kusikia maneno yanayothibitisha upendo huo. Kauli rahisi kama "Nakupenda mwanangu" inaweza kumfanya mtoto ajisikie kuthaminiwa. Maneno hayo yanaweza kusemwa asubuhi anapoondoka kwenda shule, wakati wa kulala au mnapokuwa pamoja.

Upendo haupaswi kuwa jambo ambalo mtoto analazimika kulibashiri. Na wakati mwingine, maneno mazuri yana nguvu zaidi yanapotamkwa mbele ya watu wengine.

Fikiria mtoto anayemsikia baba yake akimwambia mgeni, "Mwanangu amenisaidia sana leo kupanga vitu nyumbani."

Mtoto naye anataka kuwa na mchango

Wazazi mara nyingi huwafanyia watoto karibu kila kitu. Tunawaandalia chakula, tunapanga vyumba vyao na wakati mwingine tunawazuia kushiriki shughuli kwa kuhofia wataharibu.

Lakini mtoto anapopewa nafasi ya kusaidia, anaweza kujifunza kwamba yeye pia ana mchango katika familia.

Mwombe akusaidie kupanga vijiko mezani, kukusanya midoli au kumwagilia maua, kulingana na umri na uwezo wake.

Anapomaliza, mshukuru.

Kusema "Asante kwa kunisaidia" si kupunguza mamlaka ya mzazi. Ni kumfundisha mtoto kuthamini msaada wa wengine.

Thamini juhudi, si ushindi pekee

Mtoto anaweza kufanya mazoezi ya mpira kwa bidii lakini timu yake ikashindwa. Anaweza kusoma kwa juhudi lakini asipate alama alizotarajia.

Katika nyakati hizo, anahitaji mzazi anayemtambua kwa jitihada zake, si matokeo pekee.

Badala ya kumwambia, "Kwa nini hujashinda?" unaweza kumuuliza alijifunza nini na nini angependa kuboresha.

Mtoto anapotambua kwamba juhudi zake zina thamani, anaweza kupata moyo wa kuendelea kujaribu hata mambo yanapokuwa magumu.

Na anapofanikiwa kufanya jambo dogo, usisubiri mafanikio makubwa ndipo umpongeze.

Kujifunza kufunga kamba za viatu, kusoma neno jipya au kumsaidia mwenzake ni hatua zinazostahili kutambuliwa.

Si lazima kila mafanikio yaambatane na zawadi. Wakati mwingine tabasamu na pongezi za dhati vinatosha.

Cheza naye, hata kama una shughuli nyingi

Kwa mtoto, kucheza si kupoteza muda. Ni sehemu muhimu ya kujifunza, kujenga uhusiano na kufurahia maisha.

Lakini katika familia nyingi, wazazi wanakuwa na shughuli nyingi kiasi kwamba wanakosa hata dakika chache za kucheza na watoto wao.

Mtoto anaweza kukuomba ucheze naye mara kadhaa, lakini kila wakati unamjibu, "Subiri, nina kazi."

Jaribu kutenga muda wa kucheza mpira, kuchora, kusoma hadithi au kushiriki mchezo anaoupenda. Katika dakika hizo, weka simu pembeni na mpe umakini wako.

Mtoto hahitaji ushinde kila mchezo. Anahitaji kuona kwamba unafurahia kuwa naye.

Sikiliza kabla ya kutoa majibu

Watoto hupenda kusimulia mambo yaliyowatokea shuleni, nyumbani au walipokuwa wakicheza. Wakati mwingine simulizi zao zinaweza kuonekana ndefu au zisizokuwa na umuhimu kwa mtu mzima. Lakini mtoto anapozungumza, anahitaji kujua kwamba anasikilizwa.

Usimkatize kila wakati au kukimbilia kumpa ushauri kabla hajamaliza. Mtazame, muulize maswali na mpe nafasi ya kueleza hisia zake.

Tabia hii inaweza kujenga uaminifu na kumfanya awe tayari kukueleza hata matatizo makubwa atakapokua.

Kumbatio linaweza kusema mengi

Si kila ujumbe wa upendo unahitaji maneno.

Kumkumbatia mtoto anapokuwa na huzuni, kumshika mkono anapoogopa au kumpokea kwa furaha anaporudi shuleni ni vitendo vinavyoweza kumfanya ajisikie salama.

Wavulana nao wanahitaji kuonyeshwa upendo kama wasichana. Si sahihi kuwanyima ukaribu wa kihisia kwa kudhani kwamba lazima wawe wagumu kila wakati.

Hata hivyo, heshimu hisia na mipaka ya mtoto. Si kila mtoto hupenda kukumbatiwa kila wakati.

Penda mambo anayoyapenda

Mtoto wako anaweza kupenda magari ya kuchezea, wanyama, kuchora, mpira au hadithi za kubuni.

Huenda mambo hayo hayakuvutii, lakini kwake yana maana kubwa.

Unapomuuliza kuhusu mchezo anaoupenda au kukaa naye kuchora, unamwonyesha kwamba mambo anayoyathamini yana nafasi katika maisha yako.

Huna haja ya kuwa mtaalamu wa kila kitu anachokipenda. Mara nyingi hamu ya kujifunza kutoka kwake inatosha.

Upendo unaonekana kwenye mambo ya kawaida

Wazazi hawahitaji kuwa na fedha nyingi ili kujenga kumbukumbu nzuri katika maisha ya watoto wao.

Wanaweza kutumia muda wa safari, chakula cha jioni au maandalizi ya kulala kuzungumza, kucheka na kuonyesha upendo.

MAKALA ELIMU

Na Samrath Msuya

0789 201 383

Mwalimu, kwa mbinu hizi, jenga uhusiano mzuri na wanafunzi wako

Mwalimu anaweza kuwa na elimu kubwa, uzoefu wa miaka mingi na uwezo mzuri wa kufundisha. Lakini sifa hizo pekee hazitoshi kumfanya afanikiwe darasani. Namna anavyowatendea wanafunzi wake inaweza kuamua kama watapenda masomo, watajiamini au wataichukia shule.

Fikiria mwanafunzi anayeshindwa kujibu swali darasani. Mwalimu mmoja anamkaripia na kumcheka mbele ya wenzake. Mwingine anamsikiliza, anamwelekeza na kumtia moyo ajaribu tena. Ingawa wote wanafundisha somo lilelile, athari zao kwa mwanafunzi zinaweza kuwa tofauti kabisa.

Wataalamu wa elimu wanasisitiza kuwa uhusiano mzuri kati ya mwalimu na mwanafunzi hujenga mazingira ya kuaminiana, kuheshimiana na kujifunza bila hofu. Mwanafunzi anayejisikia salama huwa tayari kuuliza maswali, kukubali makosa na kushiriki katika shughuli za darasani.

Lakini mwalimu anawezaje kujenga uhusiano huo bila kupoteza nidhamu na mamlaka yake?

Mosi, waheshimu wanafunzi wako.

Heshima haipaswi kutoka kwa mwanafunzi kwenda kwa mwalimu pekee. Mwalimu naye anapaswa kumheshimu mwanafunzi, kumsikiliza na kutambua utu wake.

Epuka kumdhalilisha mwanafunzi mbele ya wenzake, kumtukana au kumlinganisha na wengine kwa lengo la kumfedhehesha. Unapohitaji kumrekebisha, kosoa tabia au kosa lake badala ya kushambulia utu wake.

Mwanafunzi anayeheshimiwa hujifunza kuwaheshimu wengine.

Pili, wajue wanafunzi wako.

Usiwafahamu wanafunzi kwa majina na namba za mitihani pekee. Jitahidi kuelewa uwezo wao, changamoto na mambo wanayoyapenda.

Mwanafunzi anayeshindwa kufanya kazi za nyumbani huenda si mvivu. Inawezekana ana majukumu mengi nyumbani, hana vifaa vya kujifunzia au anakabiliwa na matatizo ya kifamilia.

Kumfahamu mwanafunzi kunamsaidia mwalimu kuchagua mbinu zinazolingana na mahitaji yake.

Tatu, sikiliza kabla ya kuhukumu.

Wakati mwingine mwalimu humwadhibu mwanafunzi bila kumpa nafasi ya kueleza kilichotokea. Tabia hii inaweza kujenga chuki na kuvunja uaminifu.

Mwanafunzi anapokosea, msikilize kwanza. Haimaanishi ukubaliane na kila anachosema, bali ufanye uamuzi baada ya kuelewa mazingira ya kosa. Kusikiliza ni sehemu ya kufundisha, si ishara ya udhaifu.

Nne, tambua juhudi, si makosa pekee.

Baadhi ya walimu huwa wepesi kuona makosa kuliko maendeleo ya wanafunzi. Mwanafunzi akikosea hukemewa, lakini akifanya vizuri hakuna anayemtambua.

Jenga utamaduni wa kupongeza juhudi na maendeleo, hata kama mwanafunzi hajafikia kiwango unachotarajia.

Kauli kama, “Leo umejitahidi kuliko jana,” inaweza kumtia moyo mwanafunzi anayepambana kuboresha matokeo yake.

Hata hivyo, pongezi ziwe za kweli na zieleze jambo alilofanya vizuri.

Tano, fanya masomo yavutie.

Mwalimu anayefundisha kwa shauku huwa na nafasi nzuri ya kuwavutia wanafunzi.

Tumia mifano inayohusiana na maisha yao, hadithi, maswali, mijadala na shughuli za vitendo. Usifanye darasa kuwa sehemu ya mwalimu kuzungumza huku wanafunzi wakisikiliza pekee. Kwa mfano, unapofundisha hesabu, unaweza kutumia mifano ya biashara sokoni. Hii huwasaidia wanafunzi kuona umuhimu wa wanachojifunza.

Sita, kuwa mwadilifu.

Upendeleo ni adui wa uhusiano mzuri darasani. Mwalimu anayewapendelea wanafunzi wenye uwezo mkubwa, watoto wa familia fulani au wale anaowapenda binafsi huweza kuwavunja moyo wengine.

Weka kanuni zinazoeleweka na uzitumie kwa haki. Usimwadhibu mwanafunzi mmoja kwa kosa ambalo mwingine unampuuza.

Haki hujenga uaminifu, na uaminifu huimarisha nidhamu.

Saba, kubali makosa yako.

Mwalimu si mtu asiyeweza kukosea. Unaweza kutoa jibu lisilo sahihi, kuchelewa darasani au kumhukumu mwanafunzi kimakosa.

Unapotambua kosa, likubali na ulirekebishe. Ikiwa ulimkosea mwanafunzi, omba radhi.

Hatua hiyo haipunguzi heshima yako. Badala yake, inawafundisha wanafunzi unyenyekevu, ukweli na uwajibikaji.

Nane, wape nafasi ya kutoa maoni.

Wanafunzi si wapokeaji wa maarifa pekee. Wanaweza pia kuwa washiriki katika kuboresha ujifunzaji.

Waulize mbinu gani zinawasaidia kuelewa masomo, shughuli zipi zinawavutia na changamoto wanazokutana nazo.

Si lazima utekeleze kila pendekezo. Muhimu ni kuwaonyesha kuwa maoni yao yana thamani.

Tisa, kuwa mfano wa tabia njema.

Wanafunzi hujifunza kutokana na matendo ya walimu wao kuliko maneno pekee.

Mwalimu anayehubiri nidhamu lakini huchelewa darasani, anayetaka heshima lakini hutukana, au anayesisitiza uaminifu lakini hudanganya, anajenga mkanganyiko.

Onyesha kwa vitendo tabia unazotaka wanafunzi wajifunze.

Kumi, usidharau salamu na tabasamu.

Kumsalimia mwanafunzi kwa uchangamfu, kumwita kwa jina au kumuuliza hali yake kunaweza kuonekana jambo dogo. Lakini vitendo hivi humfanya ajisikie kutambuliwa na kuthaminiwa.


Wakati mwingine mwanafunzi anahitaji tu kujua kwamba mwalimu wake anamjali.

Hata hivyo, ukaribu huo lazima uende sambamba na mipaka ya kitaaluma, usalama wa mtoto na nidhamu.

Kuhtimisha, mwalimu bora si yule anayemaliza muhtasari wa somo pekee, bali anayejenga mazingira yanayomwezesha kila mwanafunzi kujifunza na kukua.

MAKALA YA AFYA

Na Junaynat Ally Dama



Tabia nane za kila siku zinazoweza kuathiri afya ya ubongo wako

Unaamka asubuhi na jambo la kwanza ni kushika simu. Unapitia habari zinazokutia wasiwasi, unatumia saa nyingi mbele ya kompyuta, halafu usiku unaendelea kutazama video hadi usingizi unapokuchukua.

Kesho yake unaamka umechoka, unashindwa kuwa makini kazini na wakati mwingine unasahau hata mambo madogo.

Huenda ukadhani ni uchovu wa kawaida. Lakini wataalamu wa afya wanaeleza kwamba baadhi ya mazoea yetu ya kila siku yanaweza kuathiri usingizi, kumbukumbu, umakini na afya ya akili.

Ubongo, kama viungo vingine vya mwili, unahitaji mazingira mazuri ili kufanya kazi vizuri. Si kila tabia isiyofaa husababisha uharibifu wa moja kwa moja wa ubongo, lakini baadhi yake zinaweza kuongeza hatari ya matatizo ya afya kwa muda mrefu.

Unapokaa gizani muda mrefu

Mwanga wa asili una nafasi muhimu katika kusaidia mwili kutambua wakati wa kuwa macho na wakati wa kulala.

Mtu anayekaa ndani muda mwingi bila kupata mwanga wa kutosha wa mchana anaweza kuvuruga mpangilio wake wa usingizi, hasa ikiwa pia anatumia mwanga mkali usiku.

Jitahidi kupata mwanga wa mchana, kufungua madirisha na kutumia muda nje inapowezekana. Hata matembezi mafupi ya asubuhi yanaweza kusaidia kudumisha utaratibu wa mwili.

Habari mbaya zinapokuwa chakula chako cha kila siku

Vita, ajali, mauaji, migogoro na majanga. Hizi ni baadhi ya habari zinazotawala mitandao ya kijamii.

Kufuatilia habari ni muhimu, lakini kutumia muda mwingi kusoma taarifa zinazotisha kunaweza kuongeza wasiwasi na msongo wa mawazo kwa baadhi ya watu.

Tatizo huwa kubwa zaidi unapopitia habari hizo bila kupumzika, hasa kabla ya kulala.

Weka mipaka ya muda wa kufuatilia habari. Chagua vyanzo vinavyoaminika na usijilazimishe kusoma kila taarifa inayojitokeza.

Sauti kubwa kwenye vifaa vya masikioni

Baadhi ya watu hupenda kusikiliza muziki, mihadhara au mazungumzo kwa sauti kubwa kupitia vifaa vya masikioni.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linaonya kuwa kusikiliza sauti kubwa kwa muda mrefu kunaweza kuharibu uwezo wa kusikia.

Kupoteza uwezo wa kusikia pia kumehusishwa na hatari ya kudhoofika kwa uwezo wa kufikiri katika umri mkubwa, ingawa uhusiano huo hauimaanishi kwamba kila anayetumia vifaa hivyo atapata tatizo la ubongo.

Punguza sauti na pumzisha masikio mara kwa mara.

Unapojitenga na watu

Binadamu anahitaji mahusiano ya kijamii kwa afya yake ya kihisia na kiakili.

Kujitenga na wengine kwa muda mrefu kunaweza kuongeza hatari ya upweke, msongo wa mawazo na matatizo mengine ya afya.

Tafiti pia zimehusisha kutengwa kijamii na kudhoofika kwa uwezo wa kufikiri kwa baadhi ya watu, hasa wazee.

Tafuta muda wa kuzungumza na familia, kutembelea marafiki na kushiriki shughuli za kijamii. Mazungumzo ya ana kwa ana yana thamani ambayo simu haiwezi kuibadilisha kikamilifu.

Skrini zinapoanza kutawala maisha

Simu, televisheni na kompyuta ni sehemu muhimu ya maisha ya sasa. Tatizo si teknolojia yenyewe, bali matumizi yanayoathiri shughuli nyingine muhimu.

Kutazama skrini kwa muda mrefu bila mapumziko kunaweza kuchosha macho. Kutumia simu hadi usiku wa manane kunaweza pia kuchelewesha usingizi.

Aidha, kurukaruka kutoka ujumbe mmoja kwenda mwingine kunaweza kufanya iwe vigumu kudumisha umakini katika kazi inayohitaji muda mrefu.

Panga muda wa kutumia vifaa hivi na epuka kuvifanya kuwa shughuli yako ya mwisho kabla ya kulala.

Sukari nyingi kwenye chakula

Vinywaji vyenye sukari nyingi, pipi, biskuti na vyakula vingine vitamu vinaweza kuongeza kiwango cha sukari tunachotumia kila siku bila kujitambua.

Ulaji wa sukari nyingi zilizoongezwa kwenye vyakula na vinywaji unaweza kuchangia matatizo ya kiafya kama unene na kisukari, ambavyo vina uhusiano na afya ya ubongo.

Hata hivyo, si sahihi kudai kwamba kula sukari kunaharibu kumbukumbu moja kwa moja kwa kila mtu.

Punguza vinywaji vyenye sukari nyingi na zingatia lishe yenye mboga, matunda na vyakula mbalimbali vyenye virutubisho.

Mwili unapokosa kutembea

Maisha ya sasa yamewafanya watu wengi kutumia saa nyingi wakiwa wameketi.

Tunafanya kazi kwenye kompyuta, tunasafiri kwa magari na tunapumzika mbele ya televisheni.

MAKALA SAIKOLOJIA

Na Ukhti Fatima SS

0789 201 383

Uraibu aina 6 wa kitabia unaozuia mafanikio yako

Watu wengi wanapotaja uraibu, hufikiria matumizi ya dawa za kulevya, pombe, sigara au kushindwa kuachana na simu. Lakini kuna tabia nyingine ambazo, ingawa hazionekani kuwa hatari, zinaweza kumfanya mtu ashindwe kupiga hatua maishani. Tabia hizo ni kulalamika kila wakati, kujilinganisha na wengine, kujiona huna uwezo, kujilaumu kupita kiasi, kulaumu bahati na kukataa kuukubali ukweli.

Katika saikolojia, tabia hizi zinaweza kuhusishwa na mifumo ya kufikiri inayomzuia mtu kuchukua hatua. Si uraibu kwa maana ya kitabibu, bali mazoea yanayoweza kuathiri maamuzi, kujiamini na maendeleo. Tatizo kubwa ni kwamba mtu anaweza kuishi na tabia hizi kwa miaka mingi bila kutambua kuwa zinamrudisha nyuma.

Mosi, kulalamika badala ya kutafuta suluhisho

Kila mtu hukutana na matatizo. Lakini baadhi ya watu hutumia muda mwingi kulalamikia hali zao kuliko kutafuta namna ya kuzibadilisha.

Mtu analalamikia kipato kidogo, ugumu wa maisha au kukosa fursa, lakini hachukui hatua yoyote kuboresha hali yake.

Kulalamika si kosa, hasa unapokabiliwa na dhuluma au mazingira magumu. Tatizo huanza pale malalamiko yanapochukua nafasi ya hatua.

Badala ya kujiuliza, “Kwa nini haya yananitokea mimi?” jiulize, “Ninaweza kufanya nini kuboresha hali hii?”

Huwezi kudhibiti kila kinachotokea maishani, lakini unaweza kuchukua hatua kuhusu mambo yaliyo ndani ya uwezo wako.

Pili, kujilinganisha na wengine

Una miaka 25. Rafiki yako amenunua gari. Mwingine amejenga nyumba. Wa tatu ameanzisha biashara yenye mafanikio.

Unapoangalia maisha yao, unaanza kujiona umechelewa kufanikiwa. Hili ni kosa linaloweza kukuondolea furaha na kukufanya usithamini maendeleo yako mwenyewe.

Kila mtu ana mazingira, fursa, changamoto na muda wake wa kufikia malengo.

Badala ya kuumia kwa mafanikio ya wengine, jifunze kutoka kwao. Jiulize wamefanya nini tofauti na unaweza kujifunza nini.Tumia mafanikio ya wengine kama somo, si kipimo cha kujidharau.

Tatu, kujiona huna uwezo

“Siwezi kufanya hili.” “Mimi si mzuri kwenye biashara.” “Sina akili za kusoma masomo magumu.”

Maneno haya yanaweza kuonekana ya kawaida, lakini yanaporudiwa kila wakati yanaweza kuathiri namna unavyojitazama.

Mtu anayejiona hana uwezo anaweza kuacha kujaribu hata kabla hajaanza.

Badala ya kusema, “Siwezi,” sema, “Bado sijajifunza namna ya kufanya hili.”

Huhitaji kuwa na uhakika wa kufanikiwa kabla ya kuanza. Mara nyingi kujiamini hujengwa kwa kujaribu, kukosea, kujifunza na kujaribu tena.

Nne, kujilaumu kupita kiasi

Kuna tofauti kati ya kutambua makosa yako na kujichukia kwa sababu ya makosa hayo.

Baadhi ya watu hujikosoa kila wakati kuhusu mwonekano, uwezo, matokeo ya kazi au maamuzi waliyofanya zamani.

Wanapokosea, badala ya kusema, “Nimefanya kosa,” husema, “Mimi sifai.”

Mtazamo huu unaweza kudhoofisha kujiamini na kufanya mtu aogope kujaribu mambo mapya.

Jifunze kutathmini makosa yako kwa uaminifu bila kujidhalilisha. Jiulize umekosea wapi, umejifunza nini na utafanya nini tofauti wakati mwingine. Kujirekebisha kunahitaji kujitambua, si kujichukia.

Tano, kulaumu bahati kwa kila jambo

Wapo watu wanaoamini kuwa kila wanaposhindwa, sababu ni kukosa bahati.

Biashara imefeli, wanasema hawana bahati. Hawakupata ajira, wanasema nyota yao haing’ai.

Ni kweli kwamba maisha yana mambo mengi yasiyokuwa ndani ya uwezo wetu. Lakini si kila kushindwa kunatokana na bahati mbaya.

Wakati mwingine tatizo ni ukosefu wa maandalizi, taarifa, ujuzi au maamuzi yasiyofaa.

Badala ya kulaumu bahati, chunguza kilichotokea na mambo unayoweza kubadilisha.

Sita, kukataa kuukubali ukweli.

Mtu anaweza kujua kuwa biashara yake inapata hasara, lakini akaendelea kujidanganya kwamba kila kitu kiko sawa.

Mwingine anajua ana tabia inayoharibu mahusiano yake, lakini anakataa kukiri kuwa anahitaji kubadilika.

Kukwepa ukweli kunaweza kutoa faraja ya muda mfupi, lakini hakutatui tatizo.

Hatua ya kwanza ya mabadiliko ni kukubali hali halisi, hata kama ukweli huo unaumiza. Huwezi kutatua tatizo ambalo bado unajifanya halipo.

Mabadiliko yanaanzia wapi?

Tabia hizi sita zina jambo moja linaloziunganisha: zinaweza kumfanya mtu ashindwe kuona nafasi yake ya kuchukua hatua.

Suluhisho si kujilaumu kwa kila jambo wala kudhani kuwa kila tatizo lipo ndani ya uwezo wako.

Ni kujifunza kutofautisha mambo unayoweza kubadilisha na yale yasiyokuwa ndani ya uwezo wako.

Anza kwa kuukubali ukweli, kutambua wajibu wako na kuchukua hatua zinazowezekana.

Badala ya kuendelea kujiuliza, “Kwa nini mimi niko hivi?” jiulize, “Ni tabia gani ninayoendelea kufanya inayonizuia kubadilika?”

Wakati mwingine, hatua kubwa ya maendeleo huanza kwa kuacha tabia ndogo inayokurudisha nyuma.